# *Mungu Hutimiza Neno Lake*

. . .siku zilizopita. Nami ninamshukuru yule anayefanya jitihada hii kuniimbia huo nijapo, Dada Angie na Dada Gertie. Bwana awabariki. Ninapousikia huo, unaleta kumbukumbu za zamani za kale. Kabla tu ya kuondoka maskanini, tulikuwa na uamsho mkubwa, wa majira kamili ya baridi kali, wa kuhubiri juu ya Kitabu cha Ufunuo wa Bwana Yesu. Nami . . . Karibu kila Jumapili usiku wangeimba wimbo, *Endelea Kushikilia*. Asante, Dada Gertie. Na bila shaka nina furaha kwamba walituimbia huo tena usiku wa leo.

2 Dada Angie alikuwa akisema kwamba kidogo alikuwa amepwelewa na sauti. Vema, usijisikie mpweke. Nimepwelewa, pia. Lakini, asubuhi ya leo, baada ya kuwafanya watu wateseke kupitia karibu mahubiri ya saa mbili na nusu . . . Hayo yalikuwa moja ya aina yangu ndogo sana. Kwa hiyo, nilitoka nje, wakati chini kulikuwa kumelowa maji, na, bila shaka, ndivyo ninavyoambukizwa.

3 Lakini, ninapenda tu Neno, na hasa baraka za Roho Mtakatifu pamoja na Neno. Na wakati Yeye anapobariki na kusaidia, kwa urahisi siwezi kupata mahali pa kusimamia, kwa hiyo mnajua jinsi ilivyo. Sasa, labda si muda mrefu sana hivyo usiku wa leo, ambao ninapenda kuzungumza, kwa sababu ya kupwelewa kidogo na sauti, bali kumtegemea Mungu kwa baraka zetu na msaada Wake wa kiroho ambao tunauhitaji sana katika maisha yetu.

4 Na sasa, kama vile Ndugu Neville alivyotangaza, pamoja na kipindi chake, kwenye kipindi chake, hasa. Laiti kila msikilizaji angesikiliza kipindi hicho. Sasa, yeye haniambii niseme hivi. Lakini sikuwahi kubarikiwa hivyo katika kusikiliza kipindi, kama nilivyobarikiwa Jumamosi hii iliyopita. Ni wangapi waliousikia ujumbe huo? Huo ulikuwa ni kipeo. WLRP, saa tatu hadi saa tatu na nusu, kila Jumamosi asubuhi, waimbaji watatu wa Neville.

5 Nami nilikuwa nikizungumza na ndugu anayerekodi, Ndugu Leo, aliye humu chumbani. Na alijisahau sana kwa huo, hata hakuninii . . . Alisema, “Aisee, mhubiri huyu ni nani?” Amefungua redio. Naye Ndugu Gene, ama baadhi yao, walisema, “Ni Ndugu Neville. Huu ni wakati wake.” Na kwa kweli ulikuwa ni mzuri sana. Si huo tu, bali kila mmoja.

6 Nitawaambia sababu ya mimi kupenda kumsikia Ndugu Neville akizungumza. Hasa sana si kwa sababu yeye ni mhubiri mzuri, lakini kwa sababu najua kwamba anaishi kile anachohubiri. Na ningependelea uniishie mahubiri kuliko kunihubiria moja. Yatakuwa na matokeo bora zaidi.

7 Na sasa nimetangaza, nilisema itangazwe, kwamba ningezungumza, usiku wa leo, kwa dakika chache: *Mungu Hutimiza Neno Lake.*

8 Na asubuhi ya leo, nilikuwa nikizungumza juu ya: *Uigaji Wa Ukristo.*

9 Na, sasa, Bwana na aongeze baraka Zake sasa tunaliposoma Neno Lake. Nami ninataka kusoma kutoka sehemu kadhaa katika Maandiko, angalau tatu, ama labda kunukuu zingine. Kwa sababu, Neno ndilo tunalonena habari zake. Katika Kitabu cha mwisho cha Biblia, Kitabu cha Ufunuo, baada ya Biblia nzima kuninii. . .kukamilika, hapa ulikuwa u—ujumbe kwa Kanisa. Katika mlango wa 22 wa Ufunuo, na kuanzia kifungu cha 17.

> *Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo. Naye mwenye* kiu na aseme, Njoo!. . .*Naye asikiaye na aseme, Njoo. Naye mwenye kiu na aje. Na yeye atakaye, na anywe* maji *ya uzima bure.*

> *Kwa maana namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki:*

> *Na mtu yeyote akiondoa lolote katika* maneno *ya unabii wa kitabu* hiki, *Mungu atamwondolea sehemu yake katika kitabu cha uzima, na katika ule mji mtakatifu, na katika mambo yaliyoandikwa katika kile kitabu.*

> *Yeye* mwenye kuyashuhudia *mambo haya asema, Naam, naja upesi. Amina. Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu.*

> *Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi nyote. Amina.*

10 Na halafu katika Yohana Mtakatifu, mlango wa 12 wa Yohana Mtakatifu, na kuanzia kifungu cha 39.

> *Ndiyo sababu hawakuweza kusadiki, kwa maana. . . Isaya alisema tena,*

> *Amewapofusha macho yao, na kuifanya mizito mioyo yao; wasije wakaona kwa macho, wakafahamu kwa mioyo yao, wakaongoka, nikawaponya.*

11 Na halafu katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 24, na katika kifungu cha 35, Yesu akizungumza.

> *Mbingu na nchi zitapita, bali maneno yangu hayatapita* kamwe.

12 Na katika Wagalatia 1:8.

> . . .*ijapokuwa sisi, au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo ambayo* mmeipokea, *na alaaniwe* kwenu.

13 Sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo, kwa maombi mafupi.

14 Mungu wetu, twaja Kwako katika Jina la Mwanao mpendwa, ambaye ametuamuru tuje, akisema, "Mwombeni Baba neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Kwa hiyo tunakuja, katika Jina la Yesu, kwanza kutubu dhambi zetu wenyewe na kupungukiwa kwetu; na kukuomba Wewe utusafishe na uovu wetu wote, na kuyasafisha mawazo yetu, tupate kuyawazia yaliyo mema, na yanayohusu Ufalme wa Mungu. Na jalia mawazo yetu yawe, usiku wa leo, juu ya jambo ambalo lingeuboresha Ufalme wa Mungu, na lingewaboresha watu waliomo katika Ufalme. Na mioyo yetu isafishwe na mambo yote machafu. Tunatamani kutembea sawasawa mbele Zako, kwa mikono safi na moyo safi. Na, loo, Mungu peke yake anaweza kufanya hili.

15 Nasi tunaomba, Baba, kuisafisha mikono yetu na kuitakasa mioyo yetu. Utuoshe katika maji ya farakano, kutokana na mambo ya ulimwengu, kwa Neno. Na jalia, kupitia kwa Neno, Wewe umesema, "Ninyi ni safi, kupitia kwa Neno." Nasi tunaomba kwamba Neno litachunguza kwa kina ndani ya mioyo yetu yote usiku wa leo. Na litatusafisha na kutokuamini kwokwote, mioyo yetu ipate kufanywa upya katika Roho Mtakatifu. Na jalia atuletee, usiku wa leo, mambo yale ambayo yangekuwa ya manufaa kwa Ufalme wa Mungu. Wasaidie wale, Bwana, walio—walio wanyonge safarini, wakiwa, wanaopata shida katika kuliamini Neno.

16 Na, Ee Mungu, katika saa hii ya giza na udanganyifu tunayoishi, na tunapotazamia majanga ya ulimwengu, tunaona giza pekee mbele. Nawe umesema, "Angalieni juu, mambo haya yanapoanza kutukia, kwa maana ukombozi wetu unakaribia." Pia jalia tuonywe usiku wa leo, na kwa Roho Mtakatifu, kulitia hili moyoni, kuutazama uso wa Mungu wa Mbinguni, Yeye aliyeahidi ukombozi wetu wakati huu. Na kama vile Yohana, kisiwani, alivyoomba, "Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu."

17 Nasi tunaomba ya kwamba utatujalia mambo haya, usiku wa leo. Na kuwaponya wote walio wagonjwa na wanaoteseka. Na kuwafariji watakatifu. Waite wenye dhambi wakatubu. Na utufanye upya sisi sote, tupate kuondoka hapa, tukizikaza silaha zote za Mungu, tupate kwenda kama askari waliojitayarisha kwa ajili ya vita vilivyo mbele.

18 Sasa, kama vile tumekusanyika usiku wa leo, kila mmoja katika maombi, na bendera juu yetu, Nyota ya Asubuhi ikiongoza njiani! Nalo jeshi la adui limepiga kambi pia, na mpinzani wao mkuu anatoka na kujisifu, akisema kwamba,

"Siku hizi za miujiza zimepita." Lakini, Ee Mungu, tuinulie Daudi, shujaa, mpinzani. Na jalia Roho huyo akae katika kila moyo, kwa wingi. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

19 Katika kuliendea somo hili muhimu mno, wala halilengi imani ya mtu yeyote, au kukasirisha, au kuvuruga, au kufanya adui. Limekusudiwa tu kuwakusanya na kuwaunganisha watu wa Mungu pamoja. Na sababu ya mimi kuchagua kuzungumzia maskani jambo hili usiku wa leo, ni kwa sababu ya hali ya wakati tunaoishi. Na—naamini kuwa tupo mwa—mwanzoni mwa kitu ambacho ulimwengu wote unafahamu kinakaribia kutokea. Hakuna anayeonekana kuwa na uwezo wa kuweka kidole chake juu yake tu, lakini bado tunajua kuna kitu kinachokaribia kutukia. Sio hapa tu. Ni kila mahali.

20 Nami nadhani ingefaa zaidi, usiku wa leo, kama tungechukua wakati huu, wakati watu wamekusanyika pamoja, kuongea jambo ambalo lingekuwa muhimu sana, kuboresha, kutufanya tuelewe, na kutupatia u—ufahamu bora wa Kristo na wa Injili, na wakati tunaoishi.

21 Sasa, kwanza kabisa, nataka kusema hili, ya kwamba, si muda mrefu uliopita nilikuwa katika seminari ya Kilutheri. Nao hao ndugu wa Kilutheri wakaniambia, baada ya wao kuniandikia barua, ukosoaji mkali sana, mshauri wa wanafunzi. Na kuzungumza na kuniambia mambo, kwamba—kwamba nilikuwa "mpiga ramli," na mambo mengi maovu ambayo, kwa kweli, hawangeweza kuthibitisha. Kwa sababu, nilisema, "Ibilisi hawezi kuponya."

22 Sasa, kama ibilisi anaweza kuponya, yeye ni muumbaji. Na, Muumba, kuna Mmoja tu, na huyo ni Mungu. Ibilisi hawezi kuumba.

23 Ibilisi hata hayupo kila mahali. Anaweza tu kuwa mahali pamoja kwa wakati mmoja; pepo wake wapo, kila mahali. Lakini, Mungu yuko kila mahali. Ibilisi anaweza tu kuwepo mahali pamoja.

24 Mungu ni mweza yote. Ibilisi ana uwezo ulio na kikomo, yaani, mradi tu anaweza kutupa udanganyifu wake ndani. Na jambo halali pekee alilo nalo, ni kukurudisha kwenye mavumbi ya ardhi. Hicho ndicho kitu pekee alicho nacho. Na, hilo, bado, pamoja na baraka za Mungu, ahadi ya Mungu, kwa ajili ya ufufuo.

25 Kwa hivyo, Mungu ndiye Muumba pekee, na Mungu Ndiye pekee ambaye anaweza kujenga seli. Nazo seli ni uumbaji, na uumbaji hutokana tu na Mungu. Kwa hiyo, Mungu ndiye Mponyaji pekee, wala hakuna uponyaji mwingine ila uponyaji wa Kiungu.

26 Tuna madaktari maarufu wanaoweza kuweka mfupa; lakini Mungu huponya. Tuna madaktari ambao wanaweza kukatilia

mbali kidole tumbo, au kuondoa uvimbe, ambalo ni jambo sahihi tu kufanya. Lakini ni Nani anayeponya? Mungu huponya, kwa maana Yeye ndiye Muumba pekee.

27 Sasa, ndipo akasema, “Vipi kuhusu sisi, Walutheri? Je, unafikiri kwamba unatuona sisi kuwa ni Wakristo?”

28 Nikasema, “Bila shaka kabisa.” Nikasema, “Ufalme wa Mungu umekuwa kama mtu aliyepanda mahindi shambani. Ndipo asubuhi moja, alitoka nje na akaangalia, na kulikuwa na majani mawili yaliyochipuka, mapema katika majira ya kuchipua. Ndipo huyo mkulima akasema, ‘Tazama shamba langu la mahindi!’ Sasa, je, alikuwa na mahindi? Kwa uwezekano, alikuwa nayo, lakini si katika suke.”

29 Sasa, ni kama vile tu ningekupa ninii. . .Uliniomba mwaloni, nami nikakupa mbegu yake. Kwa uwezekano, unao mwaloni, kwa sababu mwaloni uko kwenye hiyo mbegu. Na, basi, katika punje ya mahindi, unayo mahindi, lakini bado ni kwa uwezekano tu. Una punje. Sasa, huyo mkulima akasema, “Angalia shamba langu la mahindi. Si ni zuri? Mahindi yangu!” Aliyaita mahindi, hata hivyo, yalikuwa kwenye chipukizi.

30 Muda si muda, bua hilo la mahindi likakua mpaka likawa shada. Shada ndipo ambapo chavua huja, au chavua huanguka kutoka kwenye kishada, ambayo husababisha kuzaana kwa mahindi, jinsia kati ya dume na jike. Sasa, vipi kama kishada kingeangalia nyuma na kuliambia ja—jani, “Sasa, sina uhusiano wowote nawe. Hata haupo kwenye picha. Mimi ni kitu tofauti. Mimi ni kishada. Mimi ndiye ninayetambulika. Huna shughuli nalo?” Lakini, hata hivyo, bila jani, mahindi hayawezi kutoa chavua, kwa sababu kishada huanguka kwenye jani, na hapo ndipo suke huchipukia. Na uhai ule ule ulio ndani ya ja—jani pia uko kwenye kishada.

31 Muda si muda, suke linatokea. Nalo suke linatokea, ile punje. Na, halafu, punje inaambia kishada, “Sina uhusiano wowote nawe. Hata huko kwenye picha.” Lakini isingalikuwa kwa sababu ya hicho kishada, kusingekuwa na punje.

32 Kwa hiyo jambo ni kwamba, ni, ule ubua mdogo ulikuwa ndio ule uamsho wa Kilutheri; nacho kishada kilikuwa ni ule uamsho wa Kimethodisti; nalo suke ni uamsho huu. Lakini, kwa jumla, Roho yeye yule, Uhai ule ule uliokuwa kwenye huo ubua mdogo wa mahindi, kwanza kabisa, ni uhai ule ule uliomo kwenye hiyo punje.

33 Sasa, jambo pekee ambalo wapentekoste. . .Ninamaanisha pentekoste halisi, si wale wanaojiita. Lakini, Ujumbe halisi wa kipentekoste si chochote ila ni kurejeshwa kwa Kitu kile kile kilichoingia ardhini, ambacho kimebebwa kupitia kwa Lutheri, Methodisti, Baptisti, Presbiteri. Mnaona? Sasa ndio kwanza ifikie kwenye suke. Na sasa mimi. . .

34 Ingawa ninachukia sana kutoa tamshi hili, kuvu imekuwa ikikulia juu yake. Na ninyi wakulima mnajua hiyo ni nini. Ni kitu ambacho huiga suke. Sasa, hicho ndicho tunachotaka kukata, usiku wa leo. Kwa sababu, kama huiondoi kwenye mahindi yako, itafanya shamba lote kuharibika.

35 Kwa hiyo, hilo ni jambo moja ninalotaka kuweka wazi, ya kwamba, watu wa makanisa yote ya kimadhehebu, kwa kuwa wamepitia nyakati kuu, imekuwa ni kukomaa. Na sasa kanisa liko kwenye mbegu, nalo halina budi kuzaa kitu kile kile kilichoingia ardhini. Kwa hiyo, ni Kanisa lililokomaa kabisa ambalo tunaishi ndani yake. Wala sehemu moja haiwezi kusema *hivyo* kwa sehemu hiyo nyingine, kwa kuwa waliishi vizuri katika siku zao. Na hao ndio waliokuwa shamba la mahindi machoni pa Mungu, kwa hiyo sisi hatutaki kumdhalilisha yeyote.

36 Lakini kumekuwa na baadhi ya mafundisho siku hizi, hasa sana katika matangazo maarufu ya ulimwenguni kote, ambayo yamekuwa yakilidhalilisha Neno la Mungu, na kusema, kwamba, "Mungu anaishi katika kanisa, wala si katika Neno."

37 Nilimsikia mmoja wa walimu maarufu, jioni chache zilizopita, akisema, "Kwani mliitoa wapi Biblia yenu? Nadhani ilikuwa ni Mungu akiwazia kuwaandikia Biblia huko Mbinguni, na kuwapa baadhi ya Malaika wadogo, nao wakashuka kupitia ushoroba wa Mbinguni na kuwakabidhi ninyi watu." Kisha kasema, kwamba, "Hakuna mtu angeweza kuyaishi mafundisho ya Biblia. Wala haikuwa ni ya kweli kabisa." Nao wanadai kuwa ndio mwanzo wa Kanisa.

38 Sasa, hao watu, sasa, wanaoenda kwenye kanisa hilo, ni wanaume na wanawake kama tulivyo sisi, nao hupenda, na kula, na kunywa. Na je, kuna njia yoyote ya kulizuia? Sio wakati Biblia inasema itakuwa hivi; na ni kweli.

39 Lakini, ili kuwatia moyo, kwamba nataka kujiweka wazi na dhahiri, ya kwamba ninaamini ya kwamba *Hili* ni Neno la Mungu lililo kamili, lisiloweza kukosea, lisiloghoshiwa, ambalo hakuna kitu kinachoweza kuongezewa wala kuondolewa Kwake. Ni mpango kamili wa Mungu wa Kanisa Lake. "Hakuna msingi mwingine awezao kujenga mtu yeyote, ila ule ambao umekwisha kuwekwa." Mnaliona? Ndiyo maana ninaamini katika kutokosea kwa Neno la Mungu. Nikasema, kwa mmoja wa watu hao, "Ulisema Biblia hii ilikuwa wapi, kanisa lenu? Ati kanisa lenu liliiandika Biblia hii?"

"Naam, watakatifu wetu waliiandika Biblia."

40 Nikasema, "Basi kwa nini imechukuliwa hivyo, hata ninyi ni tofauti sana siku hizi na Biblia hii?"

41 "Vema," akasema, "unaona, watu hao waliishi katika wakati mmoja, tunaishi katika wakati mwingine."

42 "Lakini," nikasema, "Mungu aliishi katika nyakati zote. Na Biblia, kama imevuviwa, Mungu asiyeweza kukosea Ndiye aliyeiandika Biblia. Naye akasema, katika Neno Lake, ya kwamba, 'Mbingu na nchi zingepita, lakini Maneno Yake hayawezi kupita kamwe.'"

43 Sasa, inatisha mno kwa mtu ambaye hakuwahi kufikiria kuona mambo haya yakikaribia. Lakini, kama ungelijua, ni kutimizwa tu kwa Maandiko. Na kadiri ninavyochukia kusema hivi huku Marekani, na mazingaombwe yetu na kadhalika tuliyo nayo katika wanazoziita huduma za kidini siku hizi, sio kuwadhalilisha, watu wa Mungu wanakaa ndani yazo, lakini nataka kusema hivi: Kwamba, imefika Marekani, ambao wameondoa na kuondoka, Wakatoliki na Waprotestanti pia, kutoka kwa mafundisho ya Neno, nao wamechukua mfumo. Na mfumo huu ni mfumo wa kiakili unaowasilisha madoido badala ya Neno. Nao Wamarekani wanavutiwa na madoido. Wamarekani wamefikia mahali pa kuabudu mungu wa kike.

44 Nina heshima kubwa na ya juu kwa wanawake. Mama yangu ni mmoja, na mke wangu, na nina binti wachanga. Na mwanamke anayedumisha nafasi yake, na ni mama wa heshima, hakuna kitu cha thamani zaidi nje ya wokovu, kwa taifa letu, kuliko mwanamke halisi.

45 Lakini, inapofikia mahali, kuabudu wanawake, basi uko nje ya mpango wa Biblia. Hakuna mpango katika Biblia wa sisi kumwabudu mwanamke yeyote, Mariamu, au Mtakatifu Sisilia. Hakuna hata chembe moja ya Maandiko kwa ajili yake. Na, kwa upande mwingine, inapinga vitu kama hivyo. Basi ni kwa nini ilikuwa, kama huu ulikuwa ndio mwanzo, hawa wanaotembea na Kristo, na iliandikwa kwa uvuvio . . . Unafikiri ningechukua neno la mtu mwingine yeyote kwake? La, bwana. *Hili* ni Neno la Milele la Mungu.

46 Sasa, mhudumu, ama kasisi aliyezungumza nami, alisema, "Mungu yuko katika kanisa Lake."

47 Nikasema, "Mungu yuko katika Neno Lake." Mungu yuko katika Neno Lake. Biblia ilisema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, huyo Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa kwetu." Mungu yuko katika Neno Lake.

48 Sasa angalia, katika Agano la Kale, walikuwa na njia mbili za kuelewa ujumbe kuwa sahihi. Kwamba nabii akitabiri, au mwotaji akiota ndoto, waliisimulia hiyo mbele ya ki—kifuko cha kifuani cha Haruni. Kifuko cha kifuani cha Haruni kilikuwa na mawe ya kuzaliwa ya wale wazee kumi na wawili katika kifuko hiki cha kifuani. Alikivaa kifuani mwake kuonyesha kwamba alikuwa kuhani mkuu wa makabila kumi na mawili ya Israeli. Nao walipokuwa wakilisimulia ono hili, au wakisimulia ndoto hii; na kama Mungu aliithibitisha, kulikuwa na Nuru

ya kimbinguni iliyokuja kwenye Urimu Thumimu hii, na kuthibitisha kwamba huo ujumbe ulikuwa wa kweli. Haijalishi jinsi ulivyoonekana kuwa halisi, haijalishi jinsi ulivyoonekana kuwa unaendana na wakati; kama hiyo Nuru ya kimbinguni kwenye Urimu Thumimu haikumulika, ulikataliwa, kwa sababu Mungu hakuwa ndani yake.

49 Nami ninasema leo, loo, nawatakeni msikie: Ujumbe wowote, haidhuru ulitoka kwa kuhani, kutoka kwa mhubiri, kutoka kwa nabii, kutoka kwa chochote kile, mtu yeyote; haidhuru ni wa kiroho jinsi gani, wadhifa wake ni upi, amefanya nini, kama amewafufua wafu, kama amewaponya wagonjwa; kama yeye ndiye askofu mkuu wa Canterbury, kama yeye ni papa wa Rumi, kama yeye ni mkuu wa dhehebu lolote mashuhuri; haijalishi ni wa rohoni jinsi gani, ingawa amenena kwa lugha, ingawa amecheza katika Roho, ingawa amehubiri Injili; haijalishi amefanya nini, kama ujumbe wake hautoki katika Biblia, ni makosa. *Hii* ndiyo Urimu Thumimu ya Mungu.

50 Biblia ilipokamilika, malaika alishuka chini, alikuwa akizungumza na Yohana. Ndipo Yesu akaja, Mwenyewe, akasema, "Mimi, Yesu, nilimtuma malaika Wangu kushuhudia mambo haya. Na sasa kifunge Kitabu hiki, lakini usikitie muhuri. Kwa maana mtu yeyote atakayeondoa chochote kutoka Kwake, ama kuongeza chochote Kwake. . . " Hilo ni Neno la Mungu.

51 Paulo, kwa kushirikiana na Roho, alisema, "Ikiwa Malaika kutoka Mbinguni," sio askofu mkuu, si papa, si kadinali, "lakini kama Malaika kutoka Mbinguni, akileta ujumbe mwingine wowote isipokuwa huu ulio hapa, na awe kwenu aliyelaaniwa."

52 Lakini sasa tunakaribia. . .Kama miaka kadhaa iliyopita, kwa Roho Mtakatifu, sikuzote nimewaambia, hapo awali. Hitler na Mussolini walipoinuka, nilisema, "Yote yatalundikana. Ukomunisti utakichukua kitu hicho chote, na kushuka kutoka kaskazini."

53 Sasa angalieni hili, enyi kanisa. Ibilisi analeta propaganda hii, wala—wala haiendani na Maandiko. Ni kuchanganya akili za watu wasio na elimu, watu wasio wa kiroho. Nasi tunaishi katika siku tukufu sana ambayo watu wowote wamewahi kuishi; na hata hivyo siku ya giza kuliko zote, kwa wasioamini, wapate. . . na wakati wa kutatanisha mno, kwao, wale wasiojua. Hauna kifani, kama siku tunayoishi. Na ni furaha iliyoje kujua kwamba nanga yako inashikilia, sasa, leo hii, tunapoukaribia katika wakati huu wa giza, mbaya.

54 Sasa, sipendi kuwataja watu, majina, lakini itabidi nitaje jina la mtu fulani sasa. Lakini, ninamwombea huyo kijana mwanamume. Nami naomba, wakati wote, kwa ajili yake. Lakini, yeye ni chombo mikononi mwa ibilisi, na huyo ni mtu huyu, Elvis Presley. Watu wameingia wazimu wa bugi-wugi,

au roki. Wamarekani wameingia. Nao wanajaribu, kwa roho iyo hiyo, kuingiza kitu hicho kanisani. Ninapenda muziki wa kanisa uchezwe kama muziki wa kanisa, wala si muziki wa roki kanisani. Lakini wanapozipata roho hizi, kuna kitu nyuma ya jambo hili, naye ibilisi anajifanya mwenyewe mpinzani.

55 Ndipo inatokea kuwa maskini mvulana huyu aliyerudi nyuma, wa Kipentekoste alisema, jinsi alivyojifunza ujanja wake wa kujinengua na kutetemeka, yeye "aliushika na kujifunza kanisani." Yeye ni mfuasi wa First Assemblies of God, Memphis, Tennessee. Mchungaji wake ni rafiki yangu.

56 Naye ni chombo cha ibilisi, cha kudanganya na kuchafua akili za matineja hawa, kwa kuwafikisha mahali mpaka... Hivi punde wametoka mahali fulani huko Canada, nafikiri waliwapeleka vijana kumi na wanne kwenye taasisi ya wendawazimu, siku chache baada ya yeye kuwa huko. Na kote nchini, lakini watu wameingia wazimu, kichaa.

57 Sababu ya wao kufanya hivyo ni kwa sababu hawajui lolote bora zaidi. Loo, laiti wangalimjua Bwana Yesu; ni bora zaidi jinsi gani! Siwahukumu; ninawasikitikia wanadamu. Na sasa si ingekuwa sawa, katika siku tunazoishi, kwamba wakati mambo yanaenda jinsi yalivyo...

58 Na sanamu ya Marekani ni msichana mrembo wa Hollywood. Wakati, yeye huongoza mwenendo wa Marekani yote. Wakati, mwache atoke amevaa mavazi yake ya kizinifu, na karibu kila mwanamke Marekani atafuata mtindo wake.

59 Ilikuwa ni u—uchungu kwangu, si muda mrefu uliopita, kusimama Rumi, wakati magazeti yalipotoa kichwa cha habari cha mwanamke huyu waliyekuwa wamemweka gazetini hivi majuzi, aliyekuwa anaenda kujifungua mtoto huko Hollywood, Mrumi. Nao wakasema, gazetini, magazetini... Ambayo, rafiki yangu, Baron von Blomberg, angeweza kuzungumza lugha saba mbalimbali na kusoma gazeti vizuri sana. Alisema, "Anaweza kuwa mungu wa kike wa Marekani, lakini hapa yeye ni kahaba wa Kirumi." Ni fedheha jinsi gani! Sasa, hawana budi kuwa na mambo kama hayo, ambayo hayana budi kutukia, ili kuambatana na roho ya siku hizi.

60 Hiyo ndiyo sababu kanisa hili linaingia na ibada ya Mariamu, ya wanawake wengine, na kadhalika. Ni roho ile ile, chini ya kiongozi wa kidini. Na hiyo ndiyo sababu inawabidi kuondoa nia yako kwenye Neno la Mungu lisiloghoshiwa, wapate kutengeneza mpango huo. Hakika.

61 Je, mnaona matatizo tuliyo nayo? Mnawaona vijana wa Kimarekani, hali waliyomo? Hao ni wanaume na wanawake wa kesho. Si ajabu Yesu alisema, "Isipokuwa siku hizi zipunguzwe, hakuna mtu ambaye angeokolewa." Kwa hiyo, ninawekea msingi mawazo yangu hapa, ya kwamba tuko kwenye wakati wa mwisho. Bwana Yesu atakuja upesi.

62 Lakini, roho ya siku hizi, loo, mnaweza kuona? Chukueni mawazo yenu. Je, mnaweza kuona kilichotokea? Kabla ya shambulizi hili kuu, linalokuja, kuleta alama ya mnyama na kutimiza Maandiko, kwa kulazimisha watu, baada ya kufanikiwa kuwashika kama ilivyo katika nchi zingine, kuwalazimisha katika mambo wasiyoyakubali, ili kusababisha kuja kwa mateso na kususia. Hivi hamwezi kuona Marekani imeyaendea madoido na mungu wa kike? Na haya ni malipo, ibilisi katika milki ya mwili, akitengeneza njia kwa hili kujiwasilisha. Amina. Natumaini mnaelewa hili. Kaeni mbali nalo. Sijali ni D.D. ngapi, Ph.D., ama chochote kilicho nyuma yake; ni uongo.

63 "Maana neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe kweli," asema Bwana. "Kwa maana mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe." Neno la Mungu la Milele linahitaji kwamba wanadamu watazaliwa mara ya pili. Chochote pungufu ya hicho, wamepotea Milele. Haijalishi unashiriki kanisa gani, au jina lako liko wapi, au ulilofanya; yamepotea. Neno la Mungu halitashindwa kamwe.

64 Sasa, hayo yatosha. Nami natumaini kwamba mnayapata katika Roho ambayo yalitolewa. Ninyi wapendwa Wakatoliki, siwadhalilishi. Ninyi ni rafiki zangu. Na kama haukuwa, ni nia gani . . . Kama nilisimama hapa, kuwapiga vita, ninapaswa kwenda madhabahuni na kuweka moyo wangu sawa na Mungu. Nimesimama hapa na uchungu moyoni, ikinibidi kulisema; lakini Roho, kulingana na Neno, ambaye ananihimiza niseme, na kulionya kundi ambalo Roho Mtakatifu ametufanya kuwa waangalizi.

65 Na kuona vipindi hivi vikuu kote nchini, vya kuidhihaki Biblia hiyo waziwazi, kasema, "Ni kama vidimbwi vya matope ambavyo unapitia. Hakuna mtu angeweza kuishi Kwake." Hiyo ni kweli, mara tu mwili unapohusika.

66 Lakini Roho Mtakatifu Ndiye anayemtawala na kumwongoza mtu. Bwana na akujalie uione hiyo tafsiri.

67 Neno la Mungu ni la kwanza, na la mwisho, na la Milele, hata milele. Mara Mungu akinena Neno, haliwezi kubadilika kamwe. Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno." Basi "Neno" ni nini? Ni wazo lililotamkwa. Baba, Mungu, akiona mpango wa ukombozi, aliutazama, na kuona yale Shetani alikuwa amefanya. Naye akawazia, Naye akaona mpango pekee; ni mawazo sasa. Lakini alipoyatamka, yakawa Neno. Na mara yanapokuwa Neno, haliwezi kufa kamwe; halina budi kuwa la Milele. Kwa maana Neno Lake haliwezi kushindwa kadiri Yeye asivyoweza. Neno Lake haliwezi kuwa bila uhai kadiri Yeye asivyoweza kuwa bila uhai. Neno Lake! Watu wa kale, katika nyakati zote, wamesoma Biblia hii. Imeyavuvia makusanyiko tangu ilipoandikwa.

68 Ningekuandikia barua, unaweza kuithamini, ukisema, "Ndugu Branham, ninaithamini barua yako." Wewe ndiye mtu pekee ambaye ilikusudiwa. Baada ya kukaa kwa muda, barua hiyo itakuwa haina faida, isipokuwa ilikuwa ni ushahidi wangu au dhidi yangu.

69 Lakini mara tu Mungu amenena, ni kwa ajili ya jamii yote ya wanadamu. Nalo ni jipya tu, usiku wa leo, kama lilivyokuwa saa ile liliponenwa. Mungu alinena na kusema, "Kristo alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Wakati Mungu, kupitia mpango Wake na nia Yake, alipolinena, Kristo aliuawa pale pale, ingawa kwa kweli hakuuawa kwa muda wa miaka elfu nne baadaye. Naye Mungu mle ndani, kwa kujua tangu zamani, aliona ni nani angeokolewa na ni nani hangeokolewa. Na hapo majina yetu yakaandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, katika kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuhusishwa na Mwana-Kondoo aliyechinjwa.

70 Nayo Biblia ilisema, katika siku za mwisho. . .Sikilizeni! "Naye mpinga-Kristo akawadanganya wote wakaao juu ya nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Dumu na Neno!

71 Sasa, nimeona, miongoni mwa ndugu zetu, na ninawaambia hili ninyi Waprotestanti kwa uchaji, si kwa chuki, si kwa kijicho, sio nipate la kusema. Ingekuwa rahisi kuzungumza juu ya jambo lingine. Lakini, hilo, najua. . .

72 Nayo Biblia inasema, "Mlinzi, kuna nini usiku?" Na kama mlinzi akimwona adui akija, akakosa kuwaonya watu, Mungu alisema angehitaji damu yao mkononi mwa huyo mlinzi. Lakini mlinzi akiwaonya, basi huyo mlinzi yuko huru.

73 Kwa hiyo, lazima nionye. Pia miongoni mwa ndugu zetu Waprotestanti, nimeona, mara nyingi, baada ya Ujumbe wangu asubuhi ya leo, juu ya roho mpya, na kisha Roho wa Mungu katika. . .Ni wangapi waliokuwa hapa asubuhi ya leo? Vema. Katika roho mpya, na Roho wa Mungu. Wengi sana wana roho mpya, bila Roho wa Mungu. Nataka hili lieleweke.

74 Siku hizi, tunapata utata mkubwa unaoendelea kati ya Waprotestanti. Na ninapoingia katika makanisa yao, inasikitisha sana wakati mwingine. Na sasa tafadhali samahani usemi huu. Lakini, kama Roho Mtakatifu. . . Kama, nimezungumza na maskini mke wangu kule nyuma, hivi majuzi. Nilipowaona binamu zangu wamelala pale, wote wawili wakiangalia, wametazamana, kwa kuwa maisha yao yamedaiwa. Mmoja akiwa na ushanga wa maombi mkononi mwake, kama Mkatoliki. Na huyo mwingine, Mbaptisti, upande huo mwingine. Wote wawili, binamu zangu. Nami nikawatazama. Nikawazia, "Ee Mungu mkuu, mambo haya

yanawezekanaje? Je, nimeshindwa? Je, kumekuwa na jambo fulani?"

75 Nikamwambia mke wangu, nikasema, "Kuna mambo mengi nisiyojua, lakini kuna mambo ambayo nayajua." Nikasema, "Tangu nikiwa mvulana mdogo, nimeuchunguza utomvu wakati wa baridi kali, majira ya kupukutika, ukishuka kutoka kwenye mti huo, na kuingia mizizini, upate kujificha na kupata joto wakati wa baridi kali. Nimeuona kwa njia ya kimbinguni, katika majira ya kuchipua, ukirudi juu, ukija pamoja na majani, na matunda. Nimeona ua, katika uzuri wake wakati wa kiangazi, likiinamisha kichwa chake wakati wa baridi kali, kwenye jalidi, na kufa; nayo mbegu inaangamia, na nyama yake inaharibika. Na kisha nimeona, katika majira ya kuchipua ya mwaka, ua hilo likiinuka." Nikasema, "Naamini. Najua yanafanya hivyo. Ninaamini ya kwamba Yule anayeitwa Yehova Mungu, ninaamini ya kwamba Yehova Mungu hufanya hivyo. Anatawala maumbile. Nimemwangalia, pamoja na msonobari, pamoja na mpapai, au kwa mbetula, na mtofaa, na kila mmoja ukitofautiana na mwingine. Na jinsi ambavyo mwanadamu, aliyeumbwa kwa njia moja na nyingine, wote wameundwa na Akili kuu, huyo alikuwa ni Mungu." Nikasema, "Najua hilo."

76 Ninaamini kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Ninaamini ya kwamba, katika mwili Wake, Yeye alikuwa Mwanadamu. Alizaliwa na mwanamke, kama tu nilivyozaliwa, lakini Damu Yake haikuwa ya mwanamke; ilikuwa ya Mungu. Naye Yehova Mungu, yule Logos, aliyeatamia juu ya nchi, (katika Ujumbe wangu asubuhi ya leo), na kumwangua mtu wa kwanza kutoka katika mavumbi ya nchi; akamtia uvuli Mariamu, na kumwatamia, kutimiza Neno Lake, na kuumba chembe chembe ya Damu iliyomleta Mwana wa Mungu aliye hai. Ninaamini, katika mwili, Yeye alikuwa Mwanadamu. Ninaamini, katika nafsi Yake, Yeye alikuwa Mungu. Alikuwa madhihirisho ya Mungu hapa duniani. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha (Yeye) ulimwengu kwa nafsi Yake." Ninaamini ya kwamba Yeye hakuwa mwanadamu wa kawaida tu, wala Yeye hakuwa nabii. Alikuwa Mungu, Imanueli. Ninaamini, kwa moyo wangu wote, hiyo kuwa ni kweli. Siwezi kuthibitisha ukweli huo, kwa sababu ninii . . . kama ningeweza, basi haingekuwa ya imani. Lakini najua miti huja na kuondoka. Najua maua huja na kuondoka. Najua maumbile yote huzunguka. Ulimwengu unaketi katika mzingo wake, kwa Nguvu fulani kuu sana.

77 Na jambo lingine ninalojua, kwamba, kwa neema ya Mungu, kuna Kitu kinachonijia, katika umbo la Malaika, Nuru. Naye huniambia mambo, kile kitakachotukia, nami ninakiona. Ninajua kuwa sio mambo ya kawaida. Ananionyesha mambo, miaka mingi ijayo, na hakuna wakati mmoja imewahi kushindwa. Ninaamini ni Mungu yeye yule aliyekuwa pamoja na Yusufu, aliyekuwa pamoja na Danieli, aliyekuwa pamoja

na Eliya. Ninaamini ya kwamba ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyewaongoza wana wa Israeli, kwa Nguzo ya Moto.

78 Kwa hiyo, nimeridhika kwamba kuna jambo fulani, kwamba Biblia ni ya kweli, kwa sababu kila kiumbe, kila kitu ninachokiita imani, kila kitu ninachokitazama, ambacho nisingeweza kuthibitisha, kuthibitisha kwa Biblia hii ya kwamba ni Kweli.

79 Ninamwona Yesu. Hakuwa vile Wayahudi walivyomdhania kuwa. A—alitimiza kila hitaji ambalo Masihi alipaswa kuwa. Alikuwa ni Masihi.

80 Nami naona Roho aliyekuwa juu ya watu hao pale, namwona akishuka papa hapa na kufanya jambo lile lile. Kwa hivyo, nimekuwa mwaminio thabiti katika Neno la Mungu aliye hai, haijalishi ni jambo gani la ajabu litatokea.

81 Nimeingia makanisani. Nami nasema hivi kwa heshima sasa. Ninaona ya kwamba, mara nyingi, makanisani, ninaamini watu hupata roho za wao kwa wao, badala ya Roho Mtakatifu. Unaingia kanisani na kuangalia ambapo mchungaji labda anatikisa kichwa chake; kusanyiko lote litafanya hivyo. Unaingia kanisani ambapo mchungaji anasema ana mafuta yanayotoka mkononi mwake; muda si muda wajua, kundi hilo zima linaamini hivyo, na wanayo. Nenda kanisani ambako kuna dansi nyingi na kurukaruka na kukimbia huku na huko. Siyashutumu mambo haya; ninazungumza tu kutoka kwa u—uchunguzi, kuwasilisha ja—jambo fulani kwenu. Ikiwa utapata mchungaji ambaye ana mihemko sana, kusanyiko lote litakuwa na mihemko. Ukimwona mchungaji aliye baridi na mgumu, basi kusanyiko zima litakuwa baridi na gumu. Naamini mnapokea roho ya ninyi kwa ninyi.

82 Hebu mchukue mwanamume mzuri na mwanamke mbaya, na uwaweke pamoja, mmoja atakwenda kwa mwingine. Ama atakuwa mwanamume mbaya, au mwanamke mzuri. Wewe. . . "Watu wawili hawawezi kutembea pamoja wasipokubaliana."

83 Na hebu niseme jambo hili kwa uchaji na katika Biblia. Kwa moyo wangu wote, nimejaribu kwa yote yaliyo ndani yangu, nisiwe mbishi. Kwa sababu, lile ono, ile asubuhi niliyoweka jiwe la msingi, lilisema, "Hubiri Neno. Fanya kazi ya mwinjilisti. Timiliza huduma yako. Kwa maana utakuja wakati watakapoyakataa Mafundisho yenye uzima; bali watajilimbikizia wenyewe, pamoja, wakiwa na walimu wenye masikio ya utafiti, nao watajiepusha wasisikie yaliyo Kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo."

84 Kweli ni nini? "Neno Lako ni Kweli." Yohana 17, "Watakase, Baba, kwa ajili ya Kweli; Neno Lako ni Kweli." Sasa. . .

85 Na ikiwa nina hatia, naomba Mungu anisamehe. Lakini ninajaribu kwa moyo wangu wote kuwasilisha Ne—Neno kwa watu, ili kwamba Roho ambaye angefuata, nitakaposimama

kwenye ile Hukumu, haitakuwa ni roho ya mazingaombwe ya vyura wakiruka kutoka kwa watu, au wadudu wakiruka, au kadhalika, au mafuta yakidondoka kutoka mikononi; bali atakuwa ni Roho, aliye katika Neno la Mungu aliye hai lililoandikwa katika Biblia hii, pamoja na ujuzi wa Biblia. Hilo ndilo nimejaribu sana.

86 Sasa, kuweka wazo letu dogo juu ya mhusika fulani wa Biblia. Tukimchukua mmoja, usiku wa leo, kwenda kuleta mawazo yetu pamoja, kuyaweka pamoja na kuyawasilisha kwenu; ndipo ufanye na chochote utakacho, kile ambacho Mungu anaweka moyoni mwako.

87 Hebu na turudi katika Wafalme wa Kwanza mlango wa 22, nasi tungeona jambo hili, ya kwamba kulikuwako na mtu, mfalme, jina lake Ahabu. Naye alikuwa mfalme hodari, mwanajeshi, na mtu mashuhuri; bali, mwumini vuguvugu, mkwamia mpakani. Jina lake lilikuwa Ahabu.

88 Hatimaye, nabii Eliya, ambaye alithibitishwa, nabii, alikuwa ametangaza maangamizi ya Ahabu. Miaka mingi baada ya kufa kwa Eliya, kulikuwa na nabii jina lake Mikaya. Kwa hiyo, Yehoshafati, baba yake, alikuwa mtu mwenye haki, ambaye alikuwa mfalme wa Yuda, akaja kumtembelea Ahabu, mfalme wa Israeli.

89 Naye Ahabu alikuwa na ufalme mkuu, wa kuvutia. Sasa angalieni, ufalme mkubwa wa kuvutia! Kwa maana alikuwa na maskini mke aliyejipaka rangi, jina lake Yezebeli, na kwa urahisi alikuwa amelishawishi taifa zima, isipokuwa wateule, kuziendea sanamu za taifa lake.

90 Je, ninyi, loo, ndugu, mnaweza kuona roho ya ibilisi yuyo huyo ikifanya kazi Marekani siku hizi, maskini wale Mayezebeli, ile roho ya kuwashawishi wana wa Mungu wamwache Kristo? Ninasema hivyo, si kwa mzaha. Hapa si mahali pa mizaha. Hii ni mimbara. Hapa ndipo kilipo kiti cha hukumu cha Mungu; nalo Neno ndilo hakimu wa Mungu. Au, Yeye yuko. . . Ni hukumu Yake, Neno ndilo.

91 Sasa angalieni jinsi maskini mwanamke huyu, hapana shaka alikuwa mrembo sana, lakini aliliyumbisha taifa kabisa.

92 Na leo tunayumbishwa na nini? Kumbukeni, ninabashiri hili, ya kwamba Marekani ni mpenda wanawake. Ni mwabudu wanawake. Roho iliyoko Marekani, kabisa imepagawa na wanawake. Maskini wanawake hawa wanaweza kuivamia Hollywood, wanaweza kutembea mtaani na kupeleka wanaume wengi kuzimu kuliko vyumba vyote vya baa ambavyo ungeweza kuvikusanya pamoja.

93 Na, hata hivyo, katika hali yake nzuri, yeye ni kito kwa moyo wa mwanamume, na baraka kwa Ufalme wa Mungu. Mnaliona?

94 Sasa angalieni kwa muda kidogo. Na, la, msiwe na upendeleo; tulieni tu msikilize. Acha Roho Mtakatifu na awaletee. Sasa, siku hizi, tuko katika hali hiyo kama ilivyokuwa katika wakati wa Ahabu. Vema, chochote alichosema mwanamke huyo, hivyo ndivyo Ahabu alivyofanya. Sasa, hata kanisani, wanawaabudu wanawake.

95 Si muda mrefu uliopita, hasira yangu ya haki iliibuka. Huko Meksiko, nilipomwona maskini mwanamke mdogo, niliyejua habari zake, hasa, akishuka, akitambaa juu ya maili za mawe moto. Huku baba akitembea, pamoja na mtoto mchanga mikononi mwake, hao wawili, na mmoja akimfuata mamaye. Naye, akilia, na ngozi imetoka magotini mwake, na kuikokota mikono yake kwenye miamba, na kulia. Na kila mtu akimtazama. Alikuwa ameiendea sanamu fulani, ya mwanamke fulani aliyekufa ambaye anasemekana kwamba ni mtakatifu. Wala sisemi hili kwa kukosoa. Ninalisema katika msingi wa Neno la Mungu. Ni umizimu kweli kweli, usioghoshiwa.

96 Biblia ilisema, "Hakuna mwombezi, hakuna mpatanishi, kati ya Mungu na mwanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu."

97 Ikiwa kanisa la mwanzoni lilikuwa Katoliki, basi kwa nini wamebadilika; wakati Katoliki ya mwanzoni ilipolihukumu, nayo Katoliki hii inalikubali? "Ni ulimwengu wa mwanamke." Ndivyo ilivyo roho na wito, leo. Na hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa.

98 Na ninabashiri kwamba mwanamke fulani atakuwa mwanamke mashuhuri. Enyi vijana hapa usiku wa leo, kumbukeni Ndugu Branham amesema jambo hili. Nami nililisema mwaka wa 33, nilipokuona Kuja kwa Bwana. Na jinsi ambavyo magari yangeendelea kutengenezwa kufanana na yai, mpaka hatimaye yangefikia umbo kamili la yai. Labda sehemu yenu hapa mnajua; limeandikwa kwenye karatasi za kale na kadhalika. Ile asubuhi tulipokuwa hapa kwenye hekalu dogo la Kimasoni ambapo tulikuwa na . . . ama kituo cha watoto mayatima hapa, kwenye—kwenye barabara inayofuata, ya pili kule, ambapo tulikuwa tukifanyia mkutano. Nami nikamwona mwanamke akiinuka, fidhuli jinsi alivyokuwa, na akaitawala nchi. Nami nabashiri ya kwamba mwanamke ama atakuwa Rais, au atafanya, ama atapata mamlaka makuu ya namna fulani, huku Marekani, kabla ya kuangamizwa kabisa kwa ulimwengu. Kumbukeni hilo. Nimelisema.

99 Angalieni sasa kinachotukia. Yezebeli, alimtawala Ahabu. Alimbana pande zote. Ilikuwa kwamba, maskini baba . . . Au, mama anabaki nyumbani na watoto wakati mume mlevi akiwa huko nje. Ni maskini baba sasa anayemtunza mtoto huku mwanamke mlevi akiwa huko nje. Sasa hiyo si mizaha. Huo ni ukweli. Sizungumzi juu ya watu wenye haki. La, bwana. Ninaonyesha tu roho iliyoko ulimwenguni.

100 Sasa angalieni. Je, hiki si kiinimacho kingine. . . Angalieni nyakati za Ahabu, jinsi nchi ilivyostawi. Loo, jamani! Ule wakati mkuu wa ufanisi ulikuwa unaendelea wakati huo. Jinsi Israeli ilivyositawi chini ya Ahabu, mnafiki yule, naye Yezebeli kweli ndiye aliyekuwa mtawala nyuma yake! Na hiyo ni ninii. . . Kwenu ninyi wasomi wa Biblia. Kama vile Ahabu alivyomwoa Yezebeli na kuleta ibada za sanamu katika Uyahudi, katika wakati wa giza, vivyo hivyo Uprotestanti umeolewa na Ukatoliki, na kurudisha upagani katika kanisa la Kikristo.

101 Na leo hii, kumbukeni, kanisa la Kiprotestanti liliitwa malaya, kwa maana liliitwa kahaba, pia. Kumbukeni hilo. Kwa hiyo, chungu hakiwezi kusema kuwa birika ni nyeusi. Huwezi kuruka kutoka kwenye moto, katika kaangio. . . kikaangio, uingie ndani ya moto, ili kujisaidia.

102 Lakini, hebu tuone Ukweli. Ukweli ndio tunaotaka. Sisi ni watu wanaoelekea Umilele, nasi hatuna budi kukutana na Mungu. Na hebu tuutafute Ukweli.

103 Sasa nataka muone, kama mtaweza. Kulitokea. . . Daima, Mungu alituma huko. . . Au, jambo la kwanza, Yehoshafati, mtu mwenye haki, alishuka kumtembelea Ahabu, ndipo akajiingiza katika matatizo.

104 Huwezi kuchanganya mema na mabaya pamoja, na kupata chochote kutoka humo. Huwezi kuchanganya mafuta na maji; hayatachanganyikana. Wala wewe huwezi, wenzako na washirika wako, kuwa pamoja na mambo ya dunia, na bado uishi maisha ya ushindi. Biblia ilisema, "Ondokeni kati yao, mjitenge nao, asema Bwana." Sasa, mnaona?

Nini. . . Unasema, "Vema, Ndugu Branham, na—najua."

105 Lakini, unachukua usomi wako mwenyewe; ni kinyume na Neno. Nalo Neno ni Kweli. Ninaamini Neno.

106 Sasa angalieni, Yehoshafati alishuka kwa Ahabu, na, loo, akafanya karamu kuu. Hakika. Tungeita, leo, kwa usemi wa mitaani, "karamu murwa." Naye alimwalika kila mtu. Wakachinja maksai, na kadhalika, na kondoo. Nao wakafanya karamu kubwa miongoni mwao.

Na hapo ndipo mwaminio anapopata shida.

107 "Loo, nakwambia, una akili finyu tu, mahali pale padogo pa watakatifu wanaojibingirisha. Hivyo tu. Unapaswa kuja kwenye kanisa kubwa. Unapaswa kuja. Loo, unapaswa kuona! Mchungaji wetu ana D.D., D.D., Ph.D." Unaona, "Mchungaji we—wetu! Kwaya yetu huimba kama Malaika." Hilo halina uhusiano wowote Nalo, endapo ni kinyume na BWANA ASEMA HIVI. Sasa, . . .

108 Basi walipomchinja maksai, na kufanya karamu kubwa, Ahabu alikuwa na njia mbadala katika hilo. Na nia yake

ilikuwa mbaya. Alikuwa akijaribu kufanya onyesho kubwa, apate kumnasa Yehoshafati.

109 Na hilo ndilo jambo lile lile ibilisi analojaribu kufanya siku hizi. “Naam, sisi ndio wengi.” Hakika.

110 Kanisa la Mungu daima limekuwa la wachache, hata Yesu atakapokuja. “Msiogope kundi dogo, Baba yenu ameona vema kuwapa ninyi Ufalme.” Hiyo ni kweli. Sisi ni walio wachache, lakini hiyo ni sawa. Maadamu Mungu yuko mle, bado tu wengi, kwangu mimi; nami najua ndivyo ilivyo, kwenu. Kwa kuwa, “Mungu akiwa upande wetu, ni nani awezaye kutupinga?”

111 Sasa, lakini, yeye—yeye alikuwa na nia nyuma yake. Na alipofanya hivyo, alisema, “Sasa kwa kuwa sote tuko hapa na tuna wakati mzuri sana! Je, utapanda pamoja nami kwenda Ramoth-gileadi, kupigana? Kwa sababu, hakika, Shamu wanayo huko juu, lakini Ramoth-Gileadi ni mali yangu. Ni hakika. Tunayo haki. Sisi ndio kanisa la kwanza. Tunayo haki.” Mnaliona?

112 Naye Yehoshafati akasema, “Vema, sasa, kwa kuwa tuna wakati mzuri,” kasema, “watu wangu ni kama watu wako. Mbona, sisi sote ni waaminio, kwa vyovyote vile, kwa hiyo hebu tushirikiane pamoja.” Alifanya kosa kubwa. Alifanya. Naye Yehoshafati, akiwa wa kiroho vya kutosha . . .

113 Kama vile ninavyoamini, kwa moyo wangu wote, ya kwamba ilikuwa ni mfano wa siku hizi. Hakika, mahali fulani, kwa namna fulani, Mungu ataufikisha Ujumbe kwa walio wakweli moyoni. Alisema, hapo mwanzo, Yeye angewafikishia, kwa hiyo ameweka mpango. Hebu . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] Jilainishe tu Nalo.

114 Sasa mwangalieni. Alisema, “Hakika, nitakwea pamoja nawe. Lakini,” akasema, “hebu kidogo. Ninaamini, kabla hatujaenda, tunapaswa kumwuliza Bwana. Waonaje wewe? Kama sisi sote ni waaminio, basi na tumwulize Bwana.”

115 “Vema,” Ahabu akasema, “bila shaka, hiyo ni kweli. Loo, mbona sikuwazia hilo? Hakika. Nilipaswa kuwazia hilo, wakati wote.” Kasema, “Nina manabii mia nne walio bora kuliko wote walioko nchini. Wote nimewavalisha vizuri. Wote wana D.D.D., Ph.D., na vitu vyote. Wana shirika kubwa hapa chini, manabii, kwa hiyo nitawaleta tu huku nasi tutaona watakayosema.”

116 Mnajua, hilo halikukolea kwa Yehoshafati ipasavyo. Alininii . . .

117 Kwa hiyo wakaenda wakawaleta, wale manabii wote mia nne, walioshiba vizuri, wamevalia nadhifu. Ahabu aliwalisha chakula chake mwenyewe, maana aliwaamuru kufanya vile hasa alivyosema wafanye.

118 Haya basi. Haya basi. Loo, hakika, “Tunayo makanisa mazuri hapa, maeneo makubwa sana.” Lakini, mara nyingi,

kama mhubiri angehubiri zaidi ya dakika ishirini, halmashauri ya mashemasi ingemtenga. Lakini, nawatakia heri, mtu wa Mungu hatasikiliza upuuzi huo. Kweli. Kama angeikemea dhambi sana, mbona, kusanyiko lote lingemwondosha; lakini hiyo ni kwa sababu yuko katika dhehebu. Lakini katika Kanisa la Mungu, huchaguliwi kwa kura wala kuondolewa kwa kura. Unazaliwa ndani, mara moja, Milele, daima. Mungu pekee ndiye angeweza kukuondosha; Naye aliapa kwa nafsi Yake, hatafanya hivyo kamwe. Amina. Anajua umeumbwa kwa kitu gani kabla hajakuingiza ndani. Yeye haendeshi biashara Yake ovyo ovyo kama mashirika yetu yafanyavyo, wanawapeleka, majaribio ya siku thela—thelathini, au siku sitini, au siku tisini. Yeye anajua walivyo kabla hawajapata kunena, kabla hawajaingia Kanisani. Anajua hasa wameumbwa na nini. Hiyo ndiyo sababu hawana budi kuzaliwa mara ya pili.

119 Sasa, alipowaleta wote kule chini, naye akaketi kwenye kiti chake cha enzi, huyo mwingine akaketi kwenye kiti chake cha enzi, nao wakaketi huko nje. Kisha akasema, "Walete wahubiri wote, wale manabii." Na wote wakajitokeza, na kupitia ujanja wao. Nao walikuwa na wakati mzuri sana, vema.

120 Akasema, "Sasa, hivi hawaonekani wazuri? Sikiliza lugha wanayotumia." Loo, jamani! Jinsi wangeweza kuongea vizuri, mwajua! Loo, "Aaaaa-mina," na hila hizi zote walizopitia. Na walikuwa na mchanganyiko mzima huko. Walikuwa nao wote.

121 Kwa hiyo, wakati, muda si muda mwajua, alisema, "Kwea! Bwana asema, 'Kwea!'"

122 Akasema, "Sasa unaona, Yehoshafati? Unaona, nilikuwa sahihi, hata hivyo."

123 Kwa nini? Wanajua la kusema. Afadhali wajue la kusema, la sivyo walipoteza sifa zao. Loo, naam, bwana. Mtu wa wilaya akaja, na mkuu wa jimbo, na, ninamaanisha, walitengwa na kanisa, upesi sana, iwapo hawakusema mambo mazuri kuhusu m—mkono uliokuwa ukiwalisha. Maana, yote wajuayo ni chakula cha kimwili, kwa vyovyote vile.

124 Nina furaha kuna Mkono ambao ulikuwa na makovu, ambao unalilisha Kanisa la Mungu.

125 Angalieni. Ndipo nikawaona wote wakitabiri, "Loo, naam, mfalme! BWANA ASEMA HIVI, 'Kwea!'" Na sasa, jambo la kushangaza ni kwamba, kwa kweli walikuwa wamevuviwa.

126 Lakini sasa angalieni. Lakini aina hiyo ya uvuvio haikumgusa mtu huyo wa Mungu, Yehoshafati. Alisema, "Hebu kidogo. Naamini nilifanya kosa hapa. Kuna kasoro. Sikupaswa kujichanganya katika hili." Mnaona? Maksai anajua zizi la bwana wake. Mnaona? Kuna. . .Akasema, "Ah, ah, kunradhi, Bw. Mfalme Ahabu, lakini, ah, kwani huna mmoja zaidi, nabii mwingine?"

127 Mbona, Ahabu angesema, “Vema, mia nne, kwa nia moja, na wasomi bora kuliko wote tulio nao, nao hawa hapa kwa nia moja, kasema, ‘*Haya* ndiyo mapenzi ya Mungu! *Haya* ndiyo mapenzi ya Mungu!’”

128 Akasema, “Halisikiki sawa, kwa njia fulani,” chini moyoni mwake. Amina. Loo, mko tayari? Hili hapa. Alijua hilo halikusikika kama Neno la Mungu. Akasema, “Je, hakuna mwingine tu?”

129 Sasa sikilizeni. Ahabu akasema, “Naam, tunaye mtakatifu anayejibingirisha. Tuna mmoja jina lake Mikaya. Lakini, nakwambia, ninamchukia.” Loo, naam! “Tuna mmoja zaidi, lakini yeye si wa dhehebu letu. Walimtenga muda mrefu uliopita. Yuko huko kilimani mahali fulani. Jina lake ni Mikaya.”

130 Yehoshafati akasema, “Ningependa tu kusikia anachosema.” Amina. Mnaliona? Mfano wa siku hizi. “Je, hakuna mwingine mmoja tu?”

131 Akasema, “Naam. Lakini, loo, yeye ni mlokole! Sikuzote yeye husema tu mambo mabaya kunihusu.” Angewezaje kusema jambo lingine lolote, wakati Neno la Mungu lilisema mambo mabaya juu yake! “Mbona, hata analaani shirika letu. Mbona, yeye ni mvunja kanisa. Hivyo tu. Vema, manabii walijaribu kumleta huku na kumpa digrii yake ya Kwanza, lakini, loo, asingevumilia. Alinyanyuka moja kwa moja kutoka pale. Yeye ni maskini mlokole tu.” Mnaona?

132 Yehoshafati alikuwa na Roho wa Mungu wa kutosha juu yake, kutoka kwa baba yake, akasema, “Ningependa kumsikia. Nendeni mkamlete.”

133 “Vema, ninakuonya. Ninakuonya. Yeye hutoa udenda na chochote kile. Kamwe hana uungwana walio nao jamaa hawa wengine.”

“Ningependa kumsikia.”

“Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Mgeni hawamfuati.”

134 Ilitokea kwamba Yehoshafati alikuwa mmoja wa wana-kondoo wa Mungu. Akasema, “Hilo halisikiki sawa kabisa.” Halina ninii ya kweli . . . Linachacharisha, lakini halina ule mlio. Kama shaba iliayo na upatu uvumao; halisikiki sawa. “Kama kumwaga mbaazi kwenye ngozi kavu ya ng’ombe,” kama Roy Davis alivyozoea kusema. “Halisikiki sawa kabisa.”

135 Akasema, “Hebu nimsikie jamaa huyu ambaye ni mlokole, kama mnavyomwita. Yule ambaye hatajiunga na shirika lako, na yule ambaye ana mawazo yake tu mwenyewe.” Kwa sababu, alijua mtu huyo hapana shaka alikuwa na kweli, kwa maana alijua hiyo haikuwa kweli.

Kwa hiyo, akasema, “Nitaagizia, aletwe, basi.”

136 Kwa hiyo, hao wakaingia vilimani, na kushuka uchochoroni, popote alipokuwa akihubiri, au ile misheni ndogo. Basi huyu hapa mkimbiaji anakuja.

137 Basi walipokuwa wamekwenda, loo, jamani, hivi hawakushikwa na hamaki! Mbona, hata jamaa mmoja, jina lake Zedekia, alienda na kuweka pembe juu ya kichwa chake. Loo, ndugu, alikuwa na ufunuo sawa kabisa. Alikuwa na mafuta mikononi mwake, na chochote kile. Alikuwa na wakati mzuri. Naam, bwana. "Loo, BWANA ASEMA HIVI, jinsi tutakavyoisukuma Shamu moja kwa moja hadi kwenye nchi yake, kwa pembe hizi!" Walikuwa na wakati mzuri.

Kwa hivyo mkimbiaji aliyekuja, alisema, "Mikaya?"

Akasema, "Naam."

"Je, wewe ni mwana wa Imla?"

"Naam, ndivyo."

"Je, wewe ni nabii, mtakatifu anayejibingirisha, mlokole?"

"Naam, nadhani huyo ni mimi."

"Vema, mfalme anataka kukuona."

138 "Loo, ati anataka?" Mikaya tayari alijua jambo hilo, hapana shaka. Bwana alikuwa tayari amemwelezea kusanyiko hilo lote huko chini lilikuwa linahusu nini. Kwa hiyo, akainuka.

139 Kwa hiyo, akasema, "Sasa, ngoja kidogo. Kabla hamjaanza uamsho huu, nitakwambia la kuhubiri. Sasa, wahubiri wengine wote hawahubiri kuhusu mambo haya. Usiseme chochote kuhusu mbio za farasi, wala usiseme neno kuhusu *hili,* na—na, ama *hili* na *lile,* kwa sababu, unaona, hao wahubiri wengine hawasemi hivyo." Kasema, "Sema yale yale wanayosema." Sasa, hivyo ndivyo ingekuwa siku hizi.

140 Sasa tutasema yale Maandiko yasemayo. Akasema, "Mikaya, manabii wengine walimtabiria mfalme wetu mema. Na sasa, unajua, yeye ni mwungwana," kwa maneno mengine. "Sasa lazima useme jambo lile lile yeye, wanalosema, na kutabiri mema."

141 Akasema, "Kama Mungu wangu aishivyo, nitasema tu yale ambayo ni BWANA ASEMA HIVI." Amina. Mungu atupe Mikaya wengine; dumu na Neno. Huenda hakuwa na mambo yote ya kuvutia ambayo wengine walikuwa nayo. Huenda hakuwa na digrii wale wengine walikuwa nayo, Ph.D. Huenda hakuwa na hadhi ya kijamii. Huenda hakuwa yule D.D. mkuu, mbele ya watu. Lakini alikuwa na Neno. Amina. Loo, ndivyo hivyo. Alijua Mungu angetimiza Neno Lake. Kwa hiyo akasema, "Yale tu ambayo Mungu ananiambia niseme, nitasema jambo lile lile analosema Mungu."

142 Na kama Mungu anatabiri siku hizi zijazo, anatabiri jambo hili baya, kuwaabudu wanawake, au maombezi ya watakatifu,

au ushirika wa watakatifu; kama Yeye analaani upuuzi huu wote, na mambo haya mengine. Na kusema, “Kama vile Yane na Yambre walivyopingana na Musa, ndivyo watakavyofanya hawa katika siku za mwisho.” Ninalaani jambo hilo, katika Neno la Mungu, na kusema si sahihi.

143 Dumuni na Neno. Sijali unahisi mihemko mingapi, unaweza kuruka na kupaza sauti kiasi gani, unaweza kufanya *hili*, *linginelo* kiasi gani. Ikiwa Roho wa Mungu hakuongozi kwenye maisha safi, makamilifu mbele za Mungu, lihukumu jambo hilo. Mungu angalitaka utoe mafuta, angekufanya mzeituni au kisima cha mafuta cha Texas. Hebu niwaambieni jambo fulani, Mungu ana kusudi kwa kila jambo. Dumuni na Neno. Yale Biblia isemayo, dumuni Nayo. Ni Urimu Thumimu ya Mungu.

144 Maskini Mikaya, nabii, alidumu na Neno la Mungu; akashuka kwenda kule, kwa ujasiri tu kama simba. Usiku huo Bwana alimpa ono. Alijua mahali alipokuwa amesimama. Basi angalieni. Loo, ndugu! Hao wengine walikuwa na ono, pia, lakini ono lao halikupatana na Neno la Mungu. Lakini la Mikaya lilikuwa pamoja na Neno la Mungu. Maana, Eliya, ambaye alikuwa na Neno la Mungu, yule nabii, mwonaji, alikuwa tayari amesema yale yangempata Ahabu. Basi Mikaya angewezaje kusema jambo zuri lilikuwa linaenda kutukia, wakati Neno la Mungu lilisema mabaya yangetukia? Kwa hiyo, alikuwa pamoja na Neno.

145 Ndugu, bila kujali mnara ni mrefu vipi, au jinsi watu waliovaa vizuri wanavyoenda, mchungaji ana elimu gani, ama chochote kuhusu hili, ama kile Askofu Scheen asemacho, ama mtu mwingine yeyote, kama ni kinyume na Neno hilo, kaa mbali nacho. Dumu katika Neno. Hapo ndipo mtumishi wa kweli wa Mungu anakaa, papo hapo kwenye Neno hilo. Hiyo ni kweli.

146 Mikaya alienda kule, naye akaona ono lake. Ndipo alipotabiri, na kuona ono, aliona hilo likiendana kabisa na Neno, limeumana Nalo. Alijua alikuwa na BWANA ASEMA HIVI. Akaenda hadi pale.

147 Naye akasema, “Mikaya, mwana wa Imla, je, niende Ramoth-gileadi, au nijiondoe?”

Mikaya akasema, “Kwea.”

148 Kasema, “Sasa hilo halisikiki sawa.” Hata yeye mwenyewe, alijua vizuri zaidi.

149 Na wengi wa hao watu hujiunga na mambo hayo makubwa ya kikanisa, ili tu wawe maarufu. Wanajua tofauti. Roho wa Uzima anayefanya kazi ulimwenguni, angewaambia hiyo ni tofauti, kama walikuwa na cheche yoyote ya Uhai juu yao hata kidogo. Wanafuata mambo haya ya mazingaombwe, ya vyura kuruka, na wadudu wakirukaruka, na kutetemeka, na kurukaruka, na kukimbia, na kila kitu, huku wanajua hilo ni

kinyume. Lakini wanaenda nayo kwa sababu ya mhemko. Nani anajali kuhusu mihemko?

150 Ninataka BWANA ASEMA HIVI, hiyo ni kweli, yale Neno lisemayo. Sasa, ninaamini katika dini ya moyoni. Ninaamini katika furaha, ambayo ninaweza kujua. Ninaamini katika Nguvu za Roho Mtakatifu. Ninaamini katika uponyaji wa Kiungu. Ninaamini katika madhihirisho yote ya karama, lakini hayana budi kuwekwa kwa uchaji katika ule Mwili, yakifanya kazi katika upatanifu na Neno.

151 Ninapoingia mahali na kuanza kuhubiri, kufanya wito wa madhabahuni, mwanamke anainuka na kunena kwa lugha. Naam, ni aibu jinsi gani! Ji—jinsi inavyosikitisha! Hiyo inaonyesha ya kwamba mchungaji wao hayuko kwenye Neno la Mungu, la sivyo angekomesha jambo hilo, na kusema, "Usifanye hivyo." Mnaona? Hakuna neno dhidi ya hiyo karama; inatumika vibaya. Mnaona?

152 Na mambo mengi, ningeweza kuchukua saa kadhaa nayo. Mnajua ninachozungumzia. Huo ni, kwa jumla, Ukatoliki na Uprotestanti. Lakini, dumuni katika Neno.

153 Angalieni, sasa. Naye alipoona hilo ono, alienda na kumwambia. Akasema, "Kwea."

Akasema, "Ni mara ngapi nitakusihi uniambie ukweli!"

154 Akasema, "Lakini niliwaona Israeli wametawanyika kama kondoo wasio na mchungaji."

155 Ndipo akasema, "Nilikwambia. Nilikwambia. Nilijua kile angesema, kabla hamjamleta hapa." Hiyo ni kweli. Asingeweza kusema lingine lolote. Alikuwa na Neno la Mungu, asingeweza kufanya zaidi ila kuhukumu jambo hilo.

156 Nami ninasema, usiku wa leo, kulingana na Biblia, ninalaani upuuzi huu, mhemko, ulokole, na mambo yanayosema, "Neno la Mungu, hakuna kitu Kwake; na kanisa ni sahihi," na mambo mengine yote. Ninayalaani, katika Jina la Yesu Kristo, kwa mamlaka ya Neno la Mungu. Acha mbingu na nchi zipite, lakini Neno la Mungu litabaki kuwa Kweli milele. Hiyo ni kweli.

Sasa, alisema, "Kwea ukitaka."

157 Na kulitokea nini? Jamaa huyu alikuwa na mihemko yote mikubwa, akiwa na wakati mzuri sana, alitembea huku na huko, kwa sababu alikuwa ndiye—alikuwa ndiye kiongozi wa kanisa. Alikaribia pale na kumpiga kwenye shavu, kwa mkono wake, akampiga kofi. Loo, naweza kumsikia akisema, "Wewe ni maskini, mwigaji, mtakatifu anayejibingirisha. Roho wa Mungu alienda wapi, alipotoka kwangu, alipokujia wewe?"

158 Akasema, "Unajua nilichokiona?" Akasema, "Wakati ninyi nyote mlipokuwa na wakati wenu mzuri sana hapa chini, na shamrashamra zenu kubwa, tuseme, hapa chini, kulikuwa na kitu fulani kikiendelea Mbinguni, wakati ule ule."

159 Nami nawaambia, wakati wana wapotevu wakiwa katika zizi la nguruwe, nayo Marekani inacheza chini ya mdundo wa bugi-wugi na roki, pamoja na Elvis Presley wao na "Ni Nani Anayempenda Sucy" wao, kuna mkutano Mbinguni unaoendelea sasa.

160 Akasema, "Mungu alifungua madirisha na kuniruhusu nichungulie ndani. Mlipokuwa na wakati wenu wa roki, Mungu aliniruhusu nichungulie Mbinguni, na Mle ndani nikaona kitu fulani."

Kasema, "Uliona nini?"

161 Akasema, "Niliona jeshi kuu la Mungu, Mungu, limeketi mkono wa kuume na wa kushoto. Na kulikuwako na Malaika upande mmoja na upande mwingine." Kisha akasema, "Nilipowaona Malaika, mmoja ameketi mkono mmoja na mmoja mwingine, jeshi la Mbinguni limekusanyika." Kisha akasema, "Mungu alisema, 'Nitamtuma nani kwenda huko chini?'" Loo, jamani! Sikilizeni. "'Nimtume nani huko chini, ili tuweze kumleta Ahabu kule juu kutimiza Neno Langu, ambalo lilinenwa na nabii Wangu?'"

162 Dumu na Neno, ndugu, haidhuru wana karamu ngapi za muziki wa roki, na wanacheza kanisani jinsi gani, na jinsi wanavyoiigiza kanisani, ni kiasi gani wanafanya *hivi, vile,* ama *vinginevyo*. Dumu na Neno. Hiyo ni kweli. Mungu hutimiza Neno Lake, kila wakati.

163 Angalieni. "Lakini akasema, 'Tumtume nani huko chini? Tumtume nani ashuke kule na kumleta Ahabu huko juu, kwa maana halina budi kutimizwa?'"

164 Naye akasema, "Niliona pepo wa uwongo akitokea. Kasema, 'Niache niende. Nitashuka na kuingia katika kila mmoja wa hao maaskofu, na hao manabii, na wakuu wote wa majimbo, na hao wengine wote. Nami nitawavuvia watoe unabii wa uongo, nipate kuwapandisha huko juu.'"

165 Sasa ngojeni kidogo. Ngojeni. Mko tayari? Uvuvio, uvuvio usioambatana na Biblia, ni uvuvio wa uwongo.

166 "Ndugu Branham, tunawezaje kuwa na hakika kwamba tuko sahihi? Tunaona *hili* likija. Tunaona *hili* likitokea, na mambo haya yote, na mazingaombwe." Dumuni na Neno!

167 Hakika, wote wawili walikuwa wamevuviwa. Huyu hapa jamaa mdogo, amesimama peke yake. Alikuwa amevuviwa. Hawa hapa mia nne, maaskofu wazuri, nao walikuwa wamevuviwa. Na kila mmoja akisema, "BWANA ASEMA HIVI."

"Lakini tunajuaje ni yupi aliye sahihi?" Dumuni na Neno.

168 Mikaya alikuwa na Neno, naye alijua ya kwamba uovu ulipaswa kutendewa uovu. Alijua ya kwamba unafiki, dini hiyo ya kujisingizia, upuuzi huo uliokuwa na majivuno mengi kwake,

na Yezebeli aliyejipaka rangi, na mambo haya mengine yote, ilibidi yashughulikiwe na mkono wa Mungu aliye hai. Kwa maana, nabii, Neno la Mungu, lilisema hivyo.

Unasema, "Je, nabii huyo alikuwa Neno la Mungu?" Naam, bwana.

169 Watajua. "Katika nyakati za kale na kwa njia nyingi Bwana alisema na baba zetu kwa njia ya manabii, katika siku hizi za mwisho kwa Mwanawe, Kristo Yesu." Hiyo ni kweli. Hakika, lilikuwa ni Neno la Mungu.

170 Hao hapo, walikuwa wamevuviwa, wakadhani walikuwa sahihi! Sisemi hawakuwa waaminifu. Walikuwa waaminifu. Walikuwa watu mashuhuri. Hawakuwa watu wasio na elimu. Hawakuwa watu tu hivi hivi. Walikuwa ni watu mashuhuri, waliofunzwa katika Neno, waliovuviwa. Lakini uvuvio wao haukupatana na Neno la Biblia. Hiyo ndiyo sababu Mikaya alijua walikuwa wamekosea.

171 Nayo Biblia ilisema, ya kwamba, "Katika siku ya mwisho, watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe."

172 "Mbona, unataka kuniambia, huyo mtu duni angeweza kuniambia? Mimi ni askofu. Mimi ni kiongozi wa *fulani-fulani*. Mimi ni mtu mashuhuri katika kanisa Katoliki. Mimi ndiye mashuhuri, katika Methodisti, Baptisti, ama hata katika Upentekoste. Mimi ndiye mkuu wa jimbo. Unataka kuniambia, unamruhusu mtu huyo. . . " Hiyo ni kweli. "Unataka kuniambia *hivi, vile*?"

173 Biblia ilisema, "Watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kukufuru, wasiotii, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowawapenda wa kwao, wasiojizuia, na wenye kuwadharau walio wema; wakiwa na mfano wa utauwa, kama tu walivyokuwa nao, bali wakikana Nguvu zake, Neno." Wasiponena kulingana na Hilo, hakuna Uzima ndani yao. Hiyo ni kweli. "Wenye mfano wa utauwa, bali wakizikana; hao nao mjiepushe nao. Kwa maana hawa ndio waendao nyumba kwa nyumba, pamoja na vitabu vyao vidogo na miamsho, na kadhalika, na huwaongoza wanawake wajinga waliolemewa na tamaa za namna nyingi, wakijifunza siku zote, wala wasiweze kamwe kuifikia ile Kweli."

174 Ni wa aina gani? Yambre na Yane; wana kila aina za maajabu na kila kitu. "Kama vile Yane na Yambre walivyompinga Musa, vivyo hivyo hawa wanaipinga ile Kweli: watu walioharibikiwa na akili zao, kuhusu Neno." Wakijaribu kulichukua Neno la Mungu na kulipotosha liwe kitu kingine, kuwa la kiajabu, ama shirika la kidini, au kujijengea jina kuu, au kujifanyia jina kubwa. "Hao nao mjiepushe nao." Dumu na Neno!

175 Nini kilitokea? Alisema, "Niliona pepo huyu wa uwongo akisema, 'Nitashuka, nikawavuvie. Nitawafanya watabiri

uwongo.'" Na watu hao, wakiwa tayari sana kuufurahisha umma!

176 Ee Mungu, tusaidie. Wakiwa tayari sana kuchukua hii, "Kuwa mwalimu mwenye masikio ya utafiti, watageuzwa kutoka kwenye Ukweli waziendee hadithi za uwongo," kama vile Roho Mtakatifu alivyotuonya na kutwambia, katika siku za mwisho, jinsi watakavyokuwa. Wako tayari sana kuwa maarufu, wao wenyewe, kupata redio kubwa zaidi, televisheni kubwa zaidi, au jina kuu zaidi, au mali nyingi kanisani, kitu kikubwa zaidi, pamoja na kujiinua wenyewe. Wako tayari sana kufanya hivyo, mpaka wanashindwa kuliangalia katika Neno.

177 Lakini, Mikaya alikuwa akilitazama Neno. Alikuwa na ile Kweli. Alikuwa na Neno. Angalieni, basi, alisema yale ambayo yangetukia.

178 Ndipo jamaa huyu akasogea na kumpiga kofi usoni, akasema, "Roho wa Mungu alipitia njia gani?"

179 Kasema, "Utaiona wakati umeketi kwenye chumba cha ndani, ukijificha."

180 Ahabu akasema, "Mtieni jamaa huyo gerezani. Fungeni mikutano hii yote, kwa vyovyote vile. Hatutaki tena matendo haya ya watakatifu wanaojibingirisha hapa." Usijali, inakuja. "Mtieni gerezani na mumpe mkate wa huzuni na maji ya huzuni. Ndipo nitakaporudi kwa amani, nitamshughulikia," kwa maneno mengine, "kukata kichwa chake."

181 Maskini Mikaya, akisimama juu ya Neno la Mungu, akijua ono lake. Ee Mungu! Akijua ya kwamba ono lake lilikuwa sawa kabisa na Neno la Mungu, halingeweza kushindwa. Alisema, "Ukirudi kabisa, kwa amani, Mungu hajasema nami." Amina, na amina!

182 Loo, enyi watu! Saa imechelewa. Lakini nataka kukwambia hili, rafiki yangu mpendwa. Usisikilize (kamwe) kipindi kinachokwambia *Hili* si Neno la Mungu na Kweli. Usisikilize mambo ya kiajabuajabu yoyote ambayo hayajasemwa na kubashiriwa na Bwana Yesu Kristo. Maana, Yeye, alipokuja Mwenyewe na kuwaponya wagonjwa, alifanya hivyo tu ili Neno lipate kutimizwa. Ili tu kulitimiza Neno!

183 Ametabiri yote mawili, kwa aina zote za makanisa. Katika Ufunuo, 17, ilisema, "Nikaona mwanamke, kahaba, ameketi juu ya mnyama mkubwa wa rangi nyekundu, juu ya vichwa saba." Vatikani iko kwenye vilima saba. Niliondoka huko hivi punde tu, miezi michache iliyopita. Kisha kasema, "Alikuwa mama wa makahaba," binti waliozaliwa naye. Mwanamke yeyote mbaya anaweza kuzaa binti mzuri. Lakini angalieni. Je, kahaba ni nini? Malaya. Hawa wanawake wenye sifa mbaya ni nini? Ni wanaume. . .Ni wanawake wanaozini na kuishi na wanaume wengine ambao si mume wao.

184 Nao watu hawa, makanisa haya, wanadai kuwa watumishi wa Mungu na kanisa la Mungu, nao wanavumilia na kufanya mambo ya ulimwengu. Wanafanya uasherati wa kiroho. Wanaliacha kusanyiko lao wajipake rangi, wao. . . wanawake wavae kaptura. Nao wanawaacha watoke nje na kuvaa kama ulimwengu, wala kamwe hawalilaani. Wanawaruhusu wanaume kuvuta sigara ya kijamii, au kunywa pombe. Wanawaruhusu wafanye karamu zao ndogo za kadi, na kucheza karata katika orofa ya chini, na kuwa na maonyesho na madansi kanisani, na karamu za supu na chochote kile, na kufundisha maskini theolojia duni badala ya Neno la Mungu aliye hai. Mnajua hiyo ni kweli. Ni mambo finyu, ya kitoto, ya kidondoadume, sijui-nini, ya ibilisi! Na katika Jina la Kristo, ninayalaani, kwa msingi wa Neno la Mungu, na kusema, "Ni lazima tuzaliwe upya, tuvuviwe na Roho Mtakatifu, tuzaliwe mara ya pili, tukienenda kwa unyenyekevu, na Mbele za Mungu, tupate kufaulu katika Unyakuo katika siku zijazo." Tuachane na mambo. . . ya Mungu, enyi watu, mpige magoti yenu. Enyi kanisa la Mungu, mnaodai kwamba mmeubusu u—ukingo wa baraka za Mungu, dumuni na Neno la Mungu. Na chochote kilicho kinyume Nalo, kiondokeeni mara moja, na mwendelee kusonga mbele. Nuru za jioni ziko hapa. Bwana Yesu anakuja hivi karibuni.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo.

185 Loo, kwa Siku hiyo kuu, Siku hiyo ya siku, na Kitabu hicho cha vitabu. "Na Vitabu vikafunguliwa, na kila mtu akahukumiwa sawasawa na Maneno yaliyoandikwa katika kile Kitabu."

186 Maskini rafiki yangu uliyedanganyika, sio wote. . . Naam, rafiki yangu, nanyi ambao mmejaribu bila mafanikio, na mmepigana na hewa. Kama tu vile ndege, niliona, akijaribu kukipigisha kichwa chake dirishani, kuzima taa. Alifanya nini? A—alipiga tu akili zake zikatoka. Taa iliendelea kuwaka.

187 Siku moja, kule juu kwenye Sanamu ya Uhuru, juu katika mkono mkuu, wale ndege wadogo walikuwa wamelala wamekufa kote. Nikasema, "Ilikuwaje?"

188 Yule mtu akasema, "Ku—kulikuwa na dhoruba jana usiku. Na katika hiyo dhoruba, ndege hawa wadogo waliruka kwenye mwanga. Badala ya kutumia huo mwanga waende mahali pa usalama, walijaribu kuupiga mwanga wauzime, kwa mbawa zao ndogo. Nao wakapiga akili zao zikatoka."

189 Usijaribu kuzipiga akili zako zitoke, kulifanya Neno la Mungu liseme jambo ambalo halisemi. Usijaribu kuambatana na mashirika ya jamii ya siku hizi, kwa sababu, "Kama ukiipenda dunia, ama mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hakumo ndani yako."

190 Kwa nini usichukue tu Nuru ya Injili na kuruka hadi mahali pa usalama usiku wa leo? "Loo, utulinde, Mungu."

191 Baba wa Mbinguni, kama wanaume na wanawake wanaoketi hapa, wavulana na wasichana, watu wanaoelekea Umilele, pe—petroli na nurulimwengu wa ulimwengu huu, pamoja na elementi kumi na sita mbalimbali ambazo tumeumbwa nazo. Katika miili yao kuna nafsi iliyo na thamani; mwanzo, mwanzoni.

192 Nami nakuomba Wewe, Bwana, ushughulikie sasa hivi moyo huo, nafsi hiyo, ile sehemu nyororo inayoishi milele, inayotuwezesha sisi kusogea. Nami naomba ya kwamba utamwokoa kila mwenye dhambi aliyepotea, usiku wa leo. Jalia watambue, ya kwamba nguzo hizi kuu za maili tunazopita, ishara hizi zikimulika pande zote mbili za barabara, ni kuashiria tu kuonekana upesi kwa Mwenye haki, Bwana Yesu; Ambaye, kuwa rafiki Yake, kunamaanisha Uzima; kumjua, ni Uzima wa Milele. Nasi tunaweza tu kumjua kulingana na Biblia, si kwa kanisa letu; bali, kwa Kuzaliwa, Kuzaliwa upya, kuzaliwa mara ya pili.

193 Na, Baba, ninaamini, kwa moyo wangu wote, hakuna mwanadamu hapa, pamoja na mimi mwenyewe, ambaye angetaka kuhukumiwa au kwenda kuzimu. Na kwa nini tuache kitu kituzuie njiani mwetu? Kwa nini tukubali cha bandia, wakati anga zimejaa cha halisi?

194 Na wakati dunia iko katika karamu yake kubwa ya mvinyo ya Babeli, wakinywa mvinyo, ulevi, wanawake walio nusu uchi, masuria kama alivyokuwa nao Nebukadreza, kuna maandiko ya mkono yanayosogezwa ukutani. Waonaji wanayaona yakija, ambao huinuka juu kuliko mtu wa kawaida. Tunaliona kwa sababu limeandikwa katika Neno. "Hakuna maji tena, lakini ni moto wakati huu." Nasi tunaona maandiko ya mkono ukutani. Tunaona kwamba kila taifa limehukumiwa.

195 Naye Mungu atalitwaa Kanisa Lake, waliozaliwa mara ya pili. Saa yaja ambapo wale huko nyuma katika wakati wa Kilutheri, wakati wa Kimethodisti, kote katika nyakati, waliolala mauti na mioyo ya kweli, katika Mungu, wakati punje ilikuwa jani moja dogo tu, na ilipokuwa kishada, lakini kuendelea, pamoja, uhai huo utakusanywa pamoja, nao ufufuo utakuja. Hao wote watafanyiza ule Mwili mkuu mzuri wa Bwana Yesu, unaokaribia.

196 Ulisema, "Wale wanaolikataa watatupwa katika giza la nje, la kulia na kuomboleza, na kusaga meno." Baba Mungu, hakuna mtu ambaye angetaka kuwa huko.

197 Ee, utuhurehemu, ewe Mungu. Na kwa mioyo yetu iliyotubu, huku vichwa vyetu vimeelekezwa kwenye mavumbi, ulikotutoa, na ukikawia, tutarejea. Mungu, uturehemu, ninaposihi kwa ajili ya kusanyiko hili linalongojea. Baada ya Ujumbe huu usiku wa leo, ninaomba ya kwamba Utawaamsha watu kwenye utambuzi wa kusimama kwao Mbele Zako.

198 Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kuna mtu humu ndani. . .Ni wangapi, hasa, (lazima kuna wengi wenu,) ambao unatambua ya kwamba maisha yako hayaambatani na Neno la Mungu? Umesitasita sana. Umeamini nusunusu. Tena umechukua ulimwengu kidogo, na *hiki* kidogo na *kile* kidogo. Na wewe ni mgonjwa na umechoshwa nao, usiku wa leo. Loo, ulijiunga na kanisa, hiyo ni kweli; labda hukujiunga. Sijui. Lakini, mbele za Mungu, ambaye huenda tukasimama Mbele Zake kabla ya asubuhi, huenda kukawa na kombora la atomiki litakaloharibu kitu hiki chote, katika maangamizi, kabla ya mapambazuko asubuhi. Kumbukeni, ni mchana nchini Urusi sasa.

199 Alisema, "Wawili watakuwa kitandani," hapana shaka ni usiku mahali fulani atakapokuja, "mmoja atachukuliwa, mwingine ataachwa."

200 Je, umeridhika, moyoni mwako, kulingana na Neno la Mungu, umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, nayo matunda ya Roho yanafuata maisha yako, pamoja na upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, imani, upole, saburi? Je, yanakufuata?

201 Ikiwa sivyo, ungekuwa na hekima sa—sana, naomba niliweke hivyo, hata uinue mkono wako kwa Mungu, na unakubali kwamba umekosea, ukisema, "Mungu, unirehemu, na unisaidie kuwa aina ya Mkristo ambaye ungetaka niwe, kwa kunipa Roho Mtakatifu na kuniacha niishi maisha ya kumcha Mungu"? Je, unaweza tu kumwinulia Mungu mkono wako? Mungu ambariki kila mmoja. Mikono mingi, mingi sana imeinuliwa.

202 Sasa, kuna wengine ambao ungependa kuinua mkono wako, ambaye hukufanya hivyo wakati huo? Je, unaweza kuinua mkono wako? Wanawake. . .Mungu awabariki. Wanaume, wanawake, je, kweli mna-,. . .Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, dada. Mungu akubariki, mvulana mdogo.

203 Je, unatambua huo, uzito wa jambo hili? Huji kanisani kusikia tu Ujumbe. . .au kuona mjumbe, namaanisha. Unakuja kusikia Ujumbe. Nao Ujumbe, ni, Roho Mtakatifu akilichukua Neno la Mungu na kukupa Hilo.

204 Sasa, vipi kuhusu hilo? Labda asubuhi itakuwa imechelewa mno. Je, uko tayari, Mbele za Mungu, kuinua mkono wako, wewe ambaye bado hujainua, na kusema, "Mungu, unirehemu. Nataka Roho Wako ndani yangu"? Kwa. . .Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki huko nyuma. Mungu akubariki, na wewe, na wewe, na wewe. Naam. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana.

205 Je, ungekuwa tayari kusema, "Mungu, ninashuka kwenye nyumba ya Mfinyanzi. Mimi ni mgonjwa na mchovu. Daima nimetaka maisha yaliyowekwa wakfu. Na, usiku wa leo,

ninashuka kwenda kwenye nyumba ya Mfinyanzi, kuweka moyo wangu chini, na kusema, 'Mungu, uvunjilie wote, na unipe moyo mpya, roho mpya, na uweke Roho Wako moja kwa moja katikati yake.' Na jalia maisha yangu yaende sawasawa na Neno Lako. Nifanye Mikaya wa siku hizi, niweze kusimama juu ya BWANA ASEMA HIVI. Na maono yangu na maisha yangu, ambayo—ambayo ninaishi mbele Zako; si mimi, bali Roho ndani yangu, anaishi maisha ambayo Biblia inahitaji. Hivyo ndivyo ninavyotaka kuwa. Ee Mungu, kwa rehema Zako, nifanye hivi"?

206 Mtu fulani sasa, ambaye hujainua mkono wako, waweza kufanya hivyo sasa? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Keti tu kimya kabisa, unapoomba sasa. Kila kichwa kimeinamishwa, kila jicho limefumbwa, kila mtu akiomba. Kwa upole tu, utamu, likubali sasa.

> . . . badiliko la haraka,
> Hakuna cha duniani kitakachodumu,
> Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
>
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Jifungie ndani pamoja na Mungu sasa.

> Wakati safari yetu imekamilika, (Loo!)
> Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
> Makao yako mazuri na yenye kung'aa ya Utukufuni,
> Nafsi yako iliyonyakuliwa itayaona! (Sasa unapaswa kufanya nini?)
>
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika! (Hilo ni Neno Lake.)
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
> Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
> Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

207 Yuko papo hapo karibu nawe.

208 Nikitazama nyuma katika wasikilizaji sasa, kwa maskini mtu mpendwa; alimwambia mpenzi wake kwaheri, hivi majuzi, kwa kitambo kidogo tu. Na mwingine aliyeketi hapa, mahali fulani, alimuaga mchumba wake, kwa muda kidogo tu. Walipokuwa wakitoka, walikuwa wameshikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Waume zao wapendwa wako hapa, usiku wa leo, wakishikilia mkono wa Mungu usiobadilika, kujua ya kwamba wapenzi watakutana tena. Lo, ingekuwaje kama hawakuwa na hilo? Loo, jenga matumaini yako juu ya mambo ya Milele!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

209 Baba yetu wa Mbinguni, wakati muziki ukivuma kwa utamu, na huu ni ujumbe. Mhubiri, Roho Mtakatifu, akituhubiria sasa kupitia kwa muziki, akitwambia la kufanya na Ujumbe huu, usiku wa leo, "Shikilia tu Neno la Mungu lisilobadilika. Mbingu na nchi zitapita, na kubadilika, lakini Neno Langu halitapita kamwe." Haliwezi kubadilika. Ni Neno la Mungu asiyebadilika.

210 "Nimelificha Neno Lako moyoni mwangu," alisema mtungazaburi, "nisije nikakutenda dhambi."

211 Kumekuwa na mikono ishirini ama thelathini iliyoinuliwa, usiku wa leo, Baba. Wanaume na wanawake wamesikia Neno, wakati, "Imani chanzo chake ni kusikia." Wamefanya uamuzi huu mmoja, unaotosheleza kwa yote, kwamba kwa msaada Wako na neema Yako, tangu saa hii na kuendelea, watakutumikia Wewe.

212 Sasa si kwa utamu, Baba, utashuka moyoni mwao? Weka Roho Wako katika roho yao mpya. Ilibidi uwape roho mpya, la sivyo kamwe wasingeinua mkono wao. Wasingelitamani. Lakini, walishuka kwenye nyumba ya Mfinyanzi, na wakakuruhusu ubadilishe hisia zao na mawazo yao. Na sasa, moyoni mwao, wamekuwa wapole.

213 Nawe ulisema, "Hakuna awezaye kuja kwangu asipovutwa na Baba Yangu." Hawangeweza kuinua mikono yao, kutoka kwa mdogo kuliko wote hadi mkubwa kuliko wote, isipokuwa Wewe ulikuwa umewaambia wafanye hivyo. Walifanya hivyo kwa sababu Wewe ulizungumza nao. Na ni Mungu, akiwaleta kwa Kristo, kama zawadi ya upendo. Walisalimisha moyo wao.

214 Nasi tunaweza kusikia sauti Yako kuu ikisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu." Si Kanisa Lako; Kanisa Lako lina Neno Lako, na halipingani na Neno Lako. "Bali yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

215 Wabariki, Baba, kwa maisha marefu, kwa Uzima wa Milele. Na uwafufue Siku ya mwisho kama ulivyoahidi. Na hii na iwe ibada kuu ya kujiweka wakfu, wakati watakatifu wa Mungu aliye hai watakaposhangilia na kufanywa upya.

216 Jalia wagonjwa, kila mmoja, kama kuna yeyote aliyepo, na waponywe. Roho Wako na adhihirishwe, kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

217 Sasa tukiwa tumeinua vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu. Nashangaa, wewe uliyeinua mkono wako, naamini ulikubali ulichosema. Lakini, pia ninaamini kwamba ulikuwa mwaminifu. Nami nakupeleka kwenye Neno la Mungu, ambalo ni Kweli.

218 Sasa kuna swali moja tu, wapi, je, ulimaanisha hilo? Kama ulimaanisha, ilikuwa ni Mungu aliyebisha moyoni mwako.

[Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Hiyo ni kweli. Sasa, ikiwa kweli ulimaanisha hivyo, basi mambo ya kale yamepita. Mungu alisema hivyo. Haiwezi kubadilika.

219 Yesu alisema, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kuwamwini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele."

220 Nafikiri, kama kweli lilitukia moyoni mwako, kwamba ungejisikia kumshukuru Mungu vya kutosha, kwamba ungependa kuja hadi kwenye madhabahu Yake hapa, na kupiga magoti na kumpa shukrani kwa yale aliyokufanyia.

221 Na huku dada akiendelea na wimbo ule ule. Ningependa kila mtu aliyeinua mkono wake, pamoja na wale ambao hawakuinua, wanaotamani wanapaswa, waje huku. Na tupige magoti na tutoe shukrani kidogo kwa Mwenyezi, kwa yale aliyotufanyia. Hiyo inathibitisha ulikuwa mwaminifu.

Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Safari yetu itakapomalizika,
Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
Makao yako mazuri na yenye kung'aa ya Utukufuni,
Nafsi yako iliyonyakuliwa itayaona!

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
Jenga matumaini yako juu ya vitu vya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Lo! *Napitia.*

222 Sasa nashangaa, tunao wachungaji na wainjilisti wengi hapa, usiku wa leo, wanaopenda kuona nafsi katika Ufalme wa Mungu, sijui, ndugu, kama ninyi, mkija hapa, mchungaji, na sijui kama ndugu wangechukua mahali pao papa hapa tutawaombea hawa wapendwa.

223 Unajua nini? Kulingana na Neno, ninalijaribu. Waliinua mikono yao kwamba wangekubali Neno la Milele la Mungu, usiku huu, na kuamini. Nami nikasema, "Sasa tuliomba."

224 Sasa angalia yale Yesu aliyosema. Hebu tuyapeleke kwenye Neno sasa. Tuna mengi ya kuvutia macho, lakini hebu tuyapeleke kwenye Neno. Yesu alisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Mungu alisema hivyo. Hilo latosha milele. "Hakuna mtu," alisema Yesu, "awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Hakuna anayepotea. "Aulaye mwili Wangu na kuinywa Damu Yangu anao Uzima wa milele, nami nitamfufua siku ya mwisho."

225 Loo, ni ajabu jinsi gani, kutazama kwenye madhabahu hii, wakati nafsi moja, ina thamani ya dunia elfu kumi. Kamwe

hawakuja kujiunga na kanisa. Walikuja kwa sababu wao ni kiungo cha Mwili wa Kristo. Walikuja hapa kutoa shukrani na kuomba. Nami naomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatia upako na kuujaza kila moyo, huku na huku kwenye madhabahu hii, usiku wa leo, kwa roho wa amani, na utamu, mnyenyekevu, ambaye atazaa matunda na haki ya Kristo, mradi tu kuna pumzi katika mwili wao, na kwenda Nyumbani, Utukufuni.

226 Naomba wainjilisti na wachungaji waje na kusimama karibu nasi, tunapoomba, tafadhalini. Kila mmoja, pasipo kujali ushirika wenu na makanisa yenu, hilo halina uhusiano wowote nalo. Tunataka tu uje, papa hapa karibu na watu hawa.

> Ninapitia, naam, ninapita . . . (Acha hiyo iwe nia ya moyo wako.)
> Nitalipa gharama, yale Wakristo wengine hufanya,
> Nitaambatana (kama Mikaya.) na wachache wa Bwana waliodharauliwa,
> Nimeanza na Yesu, nami ninapita.

> Loo, ninapitia, naam, ninapita . . .
> Nitalipa gharama, yale Wakristo wengine hufanya,
> Nitaambatana na wachache wa Bwana waliodharauliwa,
> Nimeanza na Yesu, nami ninapitia.

227 Mimi . . . Je, kuna mwingine angependa kupitia hiyo njia? "Mnanionea aibu mbele za Baba Yangu, ama mbele ya wanadamu, nitawaonea aibu asubuhi, mbele ya Malaika."

228 Je, unaona aibu mbele ya kusanyiko hili dogo usiku wa leo, kuchukua msimamo wako? Je, unaona aibu? "Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu."

> Nitaambatana, Bwana, ninapitia.
> Nimeanza na Yesu, na ninapitia.

229 Iweni tu katika maombi, kila mtu, wakati wanatoa shukrani kwa Mungu, kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao.

230 Ee Mungu, Baba na Mkombozi wa wanadamu, hawa wamekuja usiku wa leo, wakikiri kwamba hawajawekwa vya kutosha katika Mwili wa Kristo. Nao wanakuja, usiku wa leo, kuchukua nafasi zao kwa uongozi wa mkono wa Mungu, na Neno.

231 Nasi tunaomba, sasa, ya kwamba utawaweka kwenye nafasi katika Ufalme, yoyote watakayotumikia. Na wajalie, kwa nia moja, usiku wa leo, kuliamini Neno Lako takatifu. Naomba Wewe, kwa Roho Mtakatifu, useme nao, na wajalie, kwa uvuvio tu, waongozwe kwenye hiyo nafasi katika Mwili wa Kristo, ambao umewaitia.

232 Ee Mungu, jinsi tunavyokushukuru kwa ajili ya jambo hili! Haya ni matukufu machoni Pako. Inasisimua mioyo yetu kuona wanaume na wanawake ambao watapiga magoti kwa unyenyekevu madhabahuni, na kukiri makosa yao, na kuomba rehema. Wapitishe, Bwana.

233 Watumishi Wako waliotiwa mafuta, wahudumu wa Neno, wamesimama kando ya watu hawa, nami nimesimama hapa karibu na dawati hili takatifu.

234 Huu ni wakati mzuri sana. Malaika wa Mungu wamepiga kambi yao, kando ya mahali hapa, usiku wa leo. Kwa maana imeandikwa katika Neno, "Malaika wa Mungu wamefanya kituo kuwazunguka wale wamchao."

235 Na katika ulimwengu mkuu usioonekana, ambao sasa umetuzunguka, ukichochea hisia zetu kwa toba, na kuleta uovu mbele ya macho yetu, ambao tumekosea. Kwa mioyo yenye kutubu, tunasalimisha njia zetu mbaya, Bwana, na kuomba rehema ya Kiungu. Na jalia Roho Mtakatifu, ambaye ametuahidi rehema, ampe kila mmoja wetu, tunapoomba kwa unyenyekevu na kumwomba Mungu alitimize Neno Lake, na kuyatengeneza maisha yetu na tabia zetu ili zilingane na Neno Lake. Tunaomba katika Jina la Kristo.

57-0120E Mungu Hutimiza Neno Lake
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org